

**UCHANGANUZI WA MAKOSA YA KIMOFONOLOJIA KATIKA LUGHA
YA KISWAHILI MIONGONI MWA WANAFUNZI WENYE ASILI YA LUGHA
YA KIKAMBA**

KALUNGU VICTORIA KATULU

**Tasnifu iliyowasilishwa ili kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili ya
Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Pwani**


Agosti, 2020

UNGAMO

Naungama kuwa tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijawahi kamwe kuwasilishwa katika chuo kikuu chochote kile kwa minajili ya kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada yoyote ile.

Kalungu Victoria Katulu

C50/PU/3032/14

Sahihi...  Tarehe... 30th April 2021


Chuo Kikuu cha Pwani

Idhini


Tunathibitisha kwamba kazi iliyowasilishwa katika tasnifu hii ya shahada ya uzamili ilifanywa na mtahiniwa chini ya usimamizi wetu. Hakuna sehemu ya tasnifu hii ambayo itatolewa kwa namna yoyote ile bila ya kibali kutoka kwa mwandishi na Chuo kikuu cha Pwani.

Wasimamizi:

Dkt Nancy Ngowa

Sahihi...  Tarehe... 30th April 2021.....
Chuo Kikuu cha Pwani

Dkt Justus Chimoni

Sahihi...  Tarehe: ... 30th April 2021....
Chuo Kikuu cha Pwani

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mume wangu Gordon Onunga na kwa mtoto wangu Juan Onunga.

SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuyakamilisha masomo yangu ya uzamili na pia kuikamilisha ripoti hii. Pili, natoa shukrani za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt Nancy Ngowa na Dkt Justus Chimoni kwa kuniongoza na kunishauri. Hakika ufanisi huu ni kwa sababu ya msaada wao.

Nawashukuru wahadhiri wangu Prof Rocha Chimera na marehemu Prof. Karisa Beja kwa ushauri wao nilipokuwa naianza kazi hii.

Shukrani za dhati ni kwa wazazi wangu marehemu Paul Kalungu na Rose Kalungu kwa kuniwekea msingi bora wa elimu. Mlinichochea sana kuanza masomo haya japo baba hukushuhudia mwisho wake. Nitakukumbuka milele. Nawashukuru pia ndugu zangu ambao walinitia moyo kila mara. Aidha shukrani za kipekee ni kwa mume wangu Gordon Onunga kwa msaada wake usio na kipimo tangu nilipoanza kazi hii. Ulilazimika kukesha kuihariri kazi hii kila nilipozidiwa pamoja na kunitia moyo wa kuendelea licha ya changamoto nilizokumbana nazo, bila kusahahau jukumu ulilojitwika la kumwalia mtoto wetu mdogo nilipokuwa nashughulikia utafiti huu. Mungu akubariki.

Mwisho kabisa ningependa kumshukuru rafiki yangu wa dhati Mercy Gimasi kwa msaada wake mkubwa wakati nilipokuwa nyanjani kukusanya data. Mungu akubariki sana.

IKISIRI

Utafiti huu umechanganua makosa ya kimofonolojia yanayofanywa na wanafunzi wa shule za upili ambao ni wazungumzaji wa lugha ya Kikamba wanapojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Utafiti huu ulinuia kutambua makosa, kupata vyanzo vya makosa hayo na kupendekeza njia za kuyatatua.

Utafiti uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Makosa kama ilivyoasisiwa na Corder (1960). Uchanganuzi Makosa ni mtazamo ambao hutumiwa kueleza makosa yanayopatikana katika kazi za wanafunzi kwa kutambua makosa, kuyaaisha, kuonyesha visababisho vya makosapamoja na kupendekeza njia za kukabiliana nayo.

Data ilikusanywa kutoka kaunti ya Makuani wilaya ya Nzau. Aidha utafiti ulihusisha shule nne kutoka wilaya ya Nzau kaunti ya Makuani. Sampuli ya utafiti ilihusisha wanafunzi wa kidato cha pili na cha tatu waliochaguliwa kushiriki katika utafiti.

Data ilichanganuliwa kwa kutumia nadharia ya uchanganuzi makosa ya Corder (1960). Matokeo ya utafiti huuni kuwepo kwa makosa ya kimofonolojia ya uchopekaji, udondoshaji na matumizi ya sauti mbadala miongoni mwa wanafunzi wakamba wanaojifunza lugha ya Kiswahili.

ABSTRACT

This research focuses on morphophonological errors made by Kamba learners learning Kiswahili as a second language. The research aims at identifying the errors, explaining the cause of errors and recommending ways of eliminating them.

The research used the Error Analysis theory by Corder (1960) a theory that focuses on errors made by second language learners by identifying the errors, grouping the errors, explaining cause of errors and recommending ways of eliminating them.

Data was collected from four schools in Nzau subcounty, Makueni County. The research samples involved the selected form two and form three students.

Data was analysed using the Error Analysis theory by Corder ((1960). Learners were found to have made errors that were classified into three groups. Errors of Insertion, errors of omission and substitution of Kiswahili phonemes for those present in Kamba language. The cause of the errors was found to be the morphophonological differences between Kiswahili and Kamba language.

YALIYOMO

| | |
|--|------|
| Ungamo | ii |
| TABARUKU | iii |
| SHUKRANI | iv |
| IKISIRI | v |
| MAELEZO YA ISTILAHU | xi |
| VIAMBATANISHO VYA VIFUPISHO VYA MANENO | xii |
| ORODHA YA MAJEDWALI | xiii |
| ORODHA YA MICHORO | xiv |
| SURA YA KWANZA: UTANGULIZI | 1 |
| 1.1. Usuli wa Mada ya Utafiti | 1 |
| 1.2. Suala la Utafiti | 3 |
| 1.3. Madhumuni ya Utafiti | 3 |
| 1.4. Maswali ya Utafiti | 4 |
| 1.5. Upeo na Mipaka | 4 |
| 1.6. Umuhimu wa Utafiti | 4 |
| 1.7. Hitimisho | 5 |
| SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI | 6 |
| 2.1. Kitangulizi | 6 |
| 2.2. Ujifunzaji wa lugha | 6 |
| 2.3. Dhana ya Makosa | 7 |

| | |
|---|----|
| 2.3.1. Makosa | 8 |
| 2.3.2. Kuteleza | 9 |
| 2.4. Kiini cha Makosa..... | 11 |
| 2.5. Uainishaji wa Makosa | 12 |
| 2.6. Misingi ya Nadharia | 14 |
| 2.7.1. Fonolojia..... | 18 |
| 2.7.2. Mofolojia | 19 |
| 2.7.2.1. Dhana ya Neno | 21 |
| 2.8.Makosa yanayosababishwa na Athari ya Lugha ya Kwanza..... | 22 |
| 2.8 Mofofonolojia ya lugha ya Kiswahili na Kikamba | 28 |
| 2.8.1 Kitangulizi | 28 |
| 2.8.2 Fonimu za Konsonanti za Kiswahili sanifu..... | 28 |
| 2.8.3Irabu za Lugha ya Kiswahili | 29 |
| 2.8.4. Konsonanti za Lugha ya Kikamba | 30 |
| 2.8.5 Irabu za Kikamba | 32 |
| 2.8.6 Muundo wa Silabi za Kiswahili na Kikamba | 33 |
| 2.8.6.1 Silabi za lugha ya Kiswahili | 34 |
| 2.8.6.1.1Muundo wa Irabu pekee (I) | 34 |
| 2.8.6.1.2 Muundo wa Konsonanti na Vokali (KI)..... | 35 |
| 2.8.8.1.3 Muundo wa Konsonanti pekee (K) | 35 |
| 2.8.6.1.4Muundo wa Konsonanti, Konsonanti, Vokali (KKI) | 35 |
| 2.8.6.1.5 Konsonanti, konsonanti, Konsonanti Irabu (KKKI) | 35 |

| | |
|--|----|
| 2.8.6.1.6 Muundo wa nazali pekee (N) | 35 |
| 2.8.6.1.7 Muundo wa Konsonanti, Kiyeyusho na irabu (KkI) | 35 |
| 2.8.6.1.8 Muundo wa Konsonanti, Konsonanti, Kiyeyusho na Irabu (KKkI)..... | 36 |
| 2.8.6.2 Muundo wa Silabi za Kikamba | 36 |
| 2.8.6.2.1 Silabi za Irabu pekee (I) | 36 |
| 2.8.6.2.2 Silabi za konsonanti na irabu (KI)..... | 36 |
| 2.8.6.2.3 Silabi za konsonanti, konsonanti na irabu (KKI) | 36 |
| 2.8.6.2.4 Silabi za Irabu na Irabu (II) | 36 |
| 2.8.8 Kanuni za kimofonolojia za Kiswahili na Kikamba | 37 |
| 2.8.8.1 Kanuni za kimofonolojia za irabu | 37 |
| 2.8.8.2 Kanuni za kimofonolojia za konsonanti..... | 42 |
| SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI..... | 45 |
| 3.1. Kitangulizi | 45 |
| 3.2 Mkabala wa Utafiti | 45 |
| 3.3. Eneo la Utafiti | 46 |
| 3.4. Data iliyokusanywa | 46 |
| 3.5. Sampuli ya Utafiti | 47 |
| 3.6. Vifaa vya Kukusanyia Data..... | 48 |
| 3.7. Uchanganuzi wa Data..... | 49 |
| 3.8. Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti | 50 |
| 3.9. Maadili ya Utafiti | 51 |

| | |
|---|----|
| SURA YA NNE: UCHANGANUZI WA DATA NA MATOKEO | 52 |
| 4.1 Kitangulizi | 52 |
| 4.2. Makosa ya uchopekaji | 53 |
| 4.2.1. Uchopekaji wa /u/..... | 53 |
| 4.2.2 Uchopekaji wa irabu /i/ | 54 |
| 4.2.3 Uchopekaji wa /h/..... | 54 |
| 4.2.4. Uchopekaji wa {ma} | 55 |
| 4.3. Udondoshaji wa /h/..... | 56 |
| 4.3. Matumizi ya sauti mbadala..... | 57 |
| 4.3.1Matumizi ya /l/ badala ya /r/..... | 58 |
| 4.3.2 Matumizi ya /mb/ badala ya /b/..... | 58 |
| 4.4 Kutathimini kiwango cha makosa yaliyotambuliwa | 60 |
| 4.5 Njia za kukabiliana na makosa yaliyotambuliwa katika utafiti..... | 61 |
| SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO..... | 64 |
| 5.1 Kitangulizi | 64 |
| 5.2 Hitimisho | 64 |
| 5.3. Mapendekezo..... | 68 |
| MAREJELEO..... | 69 |
| Kiambatanisho 1: Fomu ya hiari ya kushiriki utafiti..... | 77 |
| Kiambatanisho 2: Mada ya insha itakayotolewa kwa wanafunzi..... | 79 |

MAELEZO YA ISTILAHU

Sarufi ni sheria, kanuni au taratibu zinazopaswa kufuatwa katika lugha.

Lugha ya taifa ni lugha iliyoteuliwa kama kitambulisho cha utamaduni na ustaarabu wa taifa zima

Lugha rasmi ni lugha ambayo imeteuliwa ili kuendesha shughuli rasmi za taifa fulani

Makosa ni kanuni ambayo inakwenda kinyume na kanuni zilizowekwa

Lugha ya kwanza ni lugha ambayo mtoto hujifunza baada ya kuzaliwa kabla ya nyingine yoyote

Lugha ya pili ni lugha ambayo mtu hujifunza baada ya kujifunza lugha ya kwanza

Lugha lengwa ni lugha ambayo mwanafunzi ananuia kujifunza

Uchanganuzi Makosa ni mtazamo ambao hutumiwa kuthibitisha makosa yanayopatikana katika lugha anayojifunza mwanafunzi

Mofonolojia ni tawi la isimu linalojishughulisha na uhusiano uliopo kati ya fonolojia na mofonolojia.

VIAMBATANISHO VYA VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---------|--|
| L1 | Lugha ya kwanza |
| L2 | Lugha ya pili |
| UM | Uchanganuzi makosa |
| K.C.P.E | Kenya Certificate of Primary Education |
| K.C.S.E | Kenya Certificate of Secondary Education |
| // | Uwakilishi wa fonimu |
| \$ | Mpaka wa silabi |
| K | konsonanti |
| I | irabu |
| { } | mabano ya mofu |
| Jedw. | Jedwali |
| Mch. | Mchoro |

ORODHA YA MAJEDWALI

| | |
|--|----|
| Jedw.2.1 Usawiri wa Konsonanti za Kiswahili kutegemea Mahali pa Kutamkia na Namna ya Kutamka..... | 29 |
| Jedw.2.2 Irabu za Kiswahili | 30 |
| Jedw.2.3 Orodha ya konsonanti za Kikamba | 31 |
| Jedw.2. 4 konsonanti za Kikamba (Kielelezo cha KItavi 1992) | 32 |
| Jedw.2.5 Orodho ya Irabu za Kikamba | 33 |
| Jedw.2.6 Vokali za Kikamba kuzingatia mwinuko na mlalo wa ulimi | 33 |
| Jedw.4. 1 Makundi na kiwango cha makosa..... | 60 |

ORODHA YA MICHORO

Mch 2.1 Irabu za Kiswahili kutegemea sehemu ya ulimi na mwinuko wa ulimi30

Mch 2.2 Kielezo cha vokali za Kikamba33

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1.Usuli wa Mada ya Utafiti

Kulingana na Guthrie (1967) na Kieti (1988) Kiswahili ni lugha ya kibantu kama ilivyo lugha ya Kikamba. Hivyo kwa kuwa lugha hizi ni za nasaba moja, zinafanana kwa kiwango fulani. Lakini kama asemavyo Massamba (1996), lugha zinaweza kuhusiana lakini kila lugha ina sauti zake pamoja na utaratibu wake wa kupanga sauti hizo. Hii ina maana kuwa lugha ya Kiswahili na ya Kikamba japokuwa ni lugha za nasaba moja kila lugha ina sauti zake pamoja na upekee wake wa utaratibu wa kupanga sauti hizo ili kuunda maneno yenye maana. Kwa hivyo lugha hizi mbili zinaweza kuathiriana iwapo miundo ya lugha moja itahamishwa kwa lugha nyingine. Lugha ya Kiswahili ni lugha ambayo ina majukumu mengi. Mathalan, kipengee cha (7)(ii) cha katiba mpya ya nchi ya Kenya ya mwaka wa 2010, kinaitaja lugha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi nchini Kenya pamoja na lugha ya Kiingereza. Hii ina maana kuwa lugha hii ya Kiswahili inatumika kuendesha shughuli rasmi za kitaifa kama mawasiliano ya kiofisi na bungeni kupitisha sheria. Aidha chini ya kipengee cha 7(i), lugha ya Kiswahili inaendelea kuhudumu kama lugha ya taifa ya nchi ya Kenya. Hivi ni kusema kuwa Kiswahili kama lugha ya taifa kinalitambulisha taifa zima la Kenyapamoja na kufanikisha mawasiliano katika taifa lenye watu wanaozungumza lugha tofauti. Aidha kwa mujibu wa Shiundu na Omulando (1992) lugha ya Kiswahili inatambulika sio tu kwa kuwa lugha ya taifa bali kama lugha ya kielimu inayofundishwa. Tume ya Elimu ya Mackay (1981), katika mfumo wake wa elimu wa 8-4-4 ulikifanya Kiswahili kuwa somo la lazimakikitahiniwa katika shule za msingi na upili katika mitihani ya kitaifa ya K.C.P.E na K.C.S.E. Kwa kuwa somo la Kiswahili linatahiniwa kila mwaka, kuna haja ya Kiswahili kusomwa na kufundishwa ipasavyo la sivyo wanafunzi wataanguka mitihani yao.

Aidha kama anavyoeleza Chebet-Choge (2012) Kiswahili kinatoa nafasi za kazi kwa watu wengi kama wahadhiri, walimu na hata watafsiri. Iwapo wanafunzi watakosa kuimudu lugha ya Kiswahili ipasavyo basi watakosa nafasi hizi za ajira. Kando na hadhi ya Kiswahili nchini Kenya, lugha hii imepata matumizi mapana na kuvuka mipaka ya nchi moja. Kwa mujibu wa Chiraghdin and Mnyampala (1978) Kiswahili ni mojawapo wa lugha zinazotambulika ulimwenguni. Kiswahili ni lingua franca ya Afrika Mashariki, Afrika ya kati na kinazungumzwa katika baadhi ya maeneo kusini mwa Afrika. Kama lingua franca lugha hii inatumika katika kufanikisha mawasiliano katika maeneo haya hasa katika shughuli za kibiashara. Kwa lugha ya Kiswahili kutekeleza majukumu haya inahitaji kuwa sanifu bila athari ya lugha za kwanza ili maelewano yasikose kutimizwa. Lugha ya Kiswahili inatangazwa katika vyombo vya habari sio tu nchini Kenya bali katika mataifa mengine kama wanavyoeleza Mulokozi (2002) na Chebet-Choge (2012). Kiswahili kinatangazwa katika idhaa mbalimbali kama BBC Kiswahili, Radio Deutsche Welle na Radio Moscow. Kama lugha ya utangazaji Kiswahili kinafanikisha mawasiliano katika jamii pana.

Ni dhahiri kwamba lugha ya Kiswahili ni muhimu na inaendelea kupata matumizi mapya kila uchao. Hata hivyo, lugha hii inakumbwa na changamoto nyingi ikiwemo athari za lugha za kwanza. Kama wanavyobaini wanaisimu na watafitikatika uwanjwa wa kiisimu wa ujifunzaji wa lugha ya pili, katika kujifunza lugha ya pili wanafunzi huathiriwa na lugha zao za kwanza. Kwa mfano Alonso Alonso (1997) katika utafiti wao walibaini kuwa katika kujifunza lugha ya Kiingereza kama lugha ya pili wanafunzi waliozungumza lugha ya Kiispania kama lugha yao ya kwanza walioathirika katika kiwango cha kifonolojia. Naye Dušková (1969) alibaini kuwa wanafunzi wa Czech waliojifunza lugha ya Kiingereza kama lugha ya pili walifanya makosa ya tahajia yaliyotokana na athari ya lugha ya Czech. Lugha ya Kiswahili kama lugha ambayo watu wengi wanajifunza kama

lugha ya pili haijajitenga na hali hii ya kuathiriwa na lugha za kwanza. Ndiposa utafiti huu unachunguza athari za kimofonolojia za lugha ya Kikamba kwa lugha ya Kiswahili kamalugha ya pili.

Aidha katika kuziainisha lugha za Kibantu Guthrie (1967) aliiweka lugha ya Kikamba katika kundi E55. Lugha ya Kikamba huzungumzwa eneo la Mashariki mwa Kenya. Kwa mujibu wa Mwove (1987) na Musau (1993) lugha ya Kikamba ina lahaja mbili kuu. Lahaja ya Kitui na lahaja ya Machakos. Kulingana na Mwove (1987) lahaja ya Kimachakos huzungumzwa maeneo ya Kilungu na Makueni. Lahaja itakayotumika katika utafiti huuni ile ya Kimachakos ambayo hutumika na wazungumzaji wa kaunti ya Makueni.

1.2.Suala la Utafiti

Utafiti huu unahusu uchanganuzi wa makosa ya kimofonolojia yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Kikamba wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Utafiti unalenga kufafanua vyanzo vya makosa hayo na kupendekeza njia za kuyatatua. Makosa ya kifonolojia ya wanafunzi wakamba yalifanyiwa utafiti na Mbula (2011). Aidha, utafiti wake haukugusia suala la mofolojia. Hali hii imeacha mwanya wa kielimu utakaozibwa kupitia utafiti huu kwa kuwa utashughulikia makosa ya kimofonolojia miongoni mwa wanafunzi wakamba wanaojifunza Kiswahili.

1.3. Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu unalenga madhumuni matatu yafuatayo:

- a) Kutambua makosa ya kimofonolojia yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Kikamba wanapojifunza lugha ya Kiswahili.
- b) Kubainisha vyanzo vya makosa ya kimofonolojia yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Kikamba wanapojifunza lugha ya Kiswahili.

c) Kupendekeza njia mbalimbali za kuyatatua makosa ya kimofonolojia yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Kikamba wanapojifunza lugha ya Kiswahili.

1.4. Maswali ya Utafiti

Utafiti uliongozwa na maswali yafuatayo:

a) Ni makosa yepi ya kimofonolojia yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Kikamba wanapojifunza lugha ya Kiswahili?

b) Makosa ya kimofonolojia miongoni mwa wanafunzi wazungumzaji lugha ya Kikamba wanaojifunza lugha ya Kiswahili yanatokana na tofauti zipi za kimofonolojia kati ya lugha ya Kikamba na ile ya Kiswahili?

c) Ni njia zipi zinaweza kutumiwa kutatua makosa ya kimofonolojia yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Kikamba wanapojifunza lugha ya Kiswahili?

1.5. Upeo na Mipaka

Utafiti huu unahusu makosa ya kimofonolojia yanayofanywa na wanafunzi wa lugha ya Kikamba wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Wanaisimu walioshughulikia makosa ya wanafunzi kama Corder (1967) wanaeleza kuwa makosa hutokea katika viwango vyote vya lugha; yaani fonolojia, morfolojia na hata sintaksia. Utafiti huu umeshughulikia makosa ya kimofonolojia. Hata hivyo mtafiti anatambua kuwa matawi ya kiisimu yanahusiana na kutegemeana katika hali tofauti kwa hivyo viwango vingine vya kiisimu vitahusishwa katika utafiti huu pale tu maelezo yake yatakapohitajika ili kutimiza malengo ya kimofonolojia ya utafiti huu.

1.6. Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unalenga kueleza mbinu mbalimbali zinazoweza kutumiwa kukabiliana na makosa yanayofanywa na wanafunzi. Hivyo utafaa kwa njia tofauti:

Kwanza kabisa, utafiti huu una umuhimu mkubwa kwa walimu wanaofundisha lugha ya Kiswahili kwa sababu wataweza kutabiri makosa yanayoweza kufanywa na wanafunzi na kukabiliana nayo kabla ya kutokea. Pia, walimu wanaofunza lugha ya Kiswahili kama L2 kwa kuzitumia mbinu zitakazopendekezwa kukabiliana na makosa hayo. Wanafunzi Wakambawanaojifunza lugha ya Kiswahili (L2) watafaidika kutokana na utafiti huu kwa kuwa wataweza kufahamu makosa ya kimofonolojia wanayofanya wanapoandika na kuweka mikakati ya kukabiliana nayo binafsi au kupitia kwa walimu wao.

Aidha utafiti huu utawafaa sana washikadau katika sekta ya elimu hasa waandalizi wa mitalaa kwa kuwa kupitia utafiti huu watatoa mwongozo wa vifaa na mbinu za kufundishia kwa walimu wa Kiswahili ili kuweza kukabiliana na makosa wanayofanya wanafunzi. Utafiti huu pia utatoa mchango kwa uwanja wa kiisimu hasa isimu ya lugha za Kiafrika hususan za Kibantu, kwa kuonyesha athari ya Kikamba kwa lugha ya Kiswahili kwa kuwa utabainisha tofauti katika lugha hizi japokuwa ni lugha za nasaba moja na kwa jinsi tofauti hizi zinasababisha makosa katika lugha ya mwanafunzi.

Mwisho kabisa, utafiti huu utatoa mchango mkubwa kwa isimu ya lugha ya Kikamba kwa kuzua elimu mpya ya makosa ya kimofonolojia yanayofanywa na wanafunzi wanapojifunza Kiswahili. Isimu ya lugha ya Kikamba itaendelezwa na utafiti huu kupitia watafiti wa baadaye wa lugha ya Kikamba watakaopenda kuurejelea.

1.7. Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia usuli wa mada kwa kueleza mambo yaliyomchochea mtafiti kufanya utafiti huu na kuweka swala la utafiti wazi. Aidha tumeeleza malengo ya utafiti pamoja na nadharia tete ya utafiti, upeo wa mipaka ya utafiti na mwisho tumeeleza umuhimu wa utafiti.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI

2.1. Kitangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya maandishi kuhusu ufafanuzi wa dhana za kimsingi katika utafiti huu, misingi ya nadharia ya utafiti, pamoja na mapitio ya tafiti za awali kuhusu mada ya utafiti.

2.2. Ujifunzaji wa lugha

Chomsky (1957) anaeleza jinsi mtu hujifunza lugha kwa kudai kuwa anapozaliwa mtu huwa na uwezo wa lugha yaani huwa na mfumo ambao huzaliwa nao kwa minanjili ya kujifunza lugha. Kulingana naye, binadamu anapozaliwa huwa ana kifaa cha upataji wa lugha ambacho anakirejelea kama *Language Acquisition Device (LAD)*. Naye (Krashen, 1981) anaeleza kuwa mtu hupata umilisi wa lugha kupitia njia mbili: Upataji wa lugha na ujifunzaji wa lugha. Kulingana na Krashen katika upataji wa lugha mtu hupata umilisi wa lugha pasipo yeye kujua kuwa kuna sheria ambazo ni sharti afuate tofauti na kujifunza lugha ambapomtu hujaribu kufuata kanuni fulani kwa kuwa anafahamu kuwa kanuni hizo zipo. Selinker and Gass (2008) wanaeleza kuwa mtu hupata lugha sawa na jinsi mtoto anavyojifunza lugha ya kwanza kwa kuwa huwa hana ufahamu kuwa anajifunza lugha. Wanachofahamu ni kuwa wanatumia lugha kuwasiliana na wanapata umilisi kamili wa lugha bila wao kufahamu kwamba wanazijua sheria za lugha hiyo.

Aidha wanaisimu wanatofautisha kati ya ujifunzaji wa lugha ya pili na lugha ya kigeni. Kwa mujibu wa Moeller na Catalano (2015) mtu hujifunza lugha ya pili katika mazingira inamozungumzwa lugha hiyo hasa katika jamii anamoishi tofauti na lugha ya kigeni ambayo mtu hujifunza katika mazingira ya nje ya jamii yake. Kulingana nao mtu hujifunza lugha ya kigeni ili aitumie nje ya jamii yake. Aidha Gass (2013) anaeleza kuwa

lugha ya kigeni huwa haina majukumu katika jamii ya mtu anayejifunza tofauti na mtu anapojifunza lugha kama lugha ya pili ambapo lugha hiyo huwa na majukumu katika jamii yake. Mfano, inaweza kuwa inatumika kufanikisha mawasiliano baina ya watu wenye lugha tofauti za kwanza. Nchini Kenya Kiswahili ni lugha ya taifa na pia lugha rasmi. Japokuwa Moeller na Catalano (2015) wanasema kuwa katika uwanja wa isimu dhana ya ujifunzaji wa lugha ya pili hutumika kurejelea pia ujifunzaji wa lugha ya kigeni na huchunguza uwezo wa binadamu kujifunza lugha zingine kando na lugha yake ya kwanza, katika utafiti huu lugha ya Kiswahili inachunguzwa kama lugha ya pili. Aidha kwa mujibu wa Selinker na Gass (2008) lugha anayojifunza mtu hurejelewa kama lugha lengwa.

2.3. Dhana ya Makosa

Corder (1967) anadai kuwa kama ilivyo katika ujifunzaji wa aina yoyote ile, watu wanapojifunza lugha ya pili hufanya makosa. Kamusi la Kiswahili Fasaha (2010) inaeleza makosa kama, jambo lisilokubalika kisheria na taratibu ya mila na desturi za jamii fulani. Kutokana na maelezo haya tunapata kuwa makosa yatasemekana kutokea iwapo kuna kutozingatia sheria zilizowekwa. Aidha kwa kuwa utafiti huu unahusu ujifunzaji wa lugha, ni muhimu kufafanua dhana ya makosa kwa muktadha wa ujifunzaji wa lugha.

Dhana hii imefafanuliwa na wanaisimu mbalimbali hasa katika uwanja wa ujifunzaji wa lugha ya pili. Dulay (1982) anaeleza makosa kama miundo ya lugha ya kimaandishi au maongezi ambayo inakiuka kanuni za lugha lengwa. Tukizingatia maelezo yao ni kwamba makosa yatasemekana kuwepo iwapo lugha ya mwanafunzi itakuwa tofauti na miundo sahihi ya lugha anayojifunza. Kwa upande wake Norrish (1987) makosa ni ukiukaji wa kanuni ambao hutokea wakati mwanafunzi hajajifunza. Hii ina maana kuwa makosa yatatokea iwapo kanuni za lugha lengwa hazijazingatiwa. Kwa upande

mwingine, Richards na Schmidt (2002:184) wanaeleza makosa kama matumizi ya lugha ambayo mzawa wa lugha itaitaja kutokuwa sahihi. Kutokana na maelezo yao ni mzawa wa lugha ya Kiswahili au mtu mwenye umilisi sawa na mzawa wa lugha lengwa anayeweza kutambua makosa.

Aidha mwanaisinu Corder (1967) katika kueleza dhana ya makosa katika ujifunzaji wa lugha ya pili alizua dhana mbili ambazo anazirejelea kwa lugha ya Kiingereza kama *errors and mistakes*. Katika utafiti huu dhana hizi zimetafsiriwa kamamakosa na *kuteleza* mtawalia. Aidha wanaisimu mbalimbali wamezitofautisha dhana hizi mbili kwa muktadha wa ujifunzaji wa lugha

2.3.1. Makosa

Kwa mujibu wa Corder (1967),(Miller, 1966),(Richards, 1974:24) na Ellis (1994) makosa hutokana na umilisi alionao mwanafunzi na huwa na ruwaza fulani. Umilisi kulingana na Holt (1975) ni ujuzi alionao mzawa wa lugha kuhusu lugha yake ujuzi ambao humwezesha kuzalisha sentensi nyingi sisizo kikomo za lugha yake. Aidha mzawa wa lugha huwa na ujuzi huu bila kufahamu kuwa anao. Hii ina maana kuwa mwanafunzi hufanya makosa kwa sababu bado hajapata ujuzi kamili wa lugha anayojifunza yaani lugha lengwa. Kulingana Holt makosa hudhihirisha kiasi cha lugha alichojifunza mwanafunzi katika lugha ya pili. Aidha anaeleza kwamba kwa kuwa makosa hutokana na umilisi basi mwanafunzi hatambui anapofanya makosa haya na binafsi hawezi kuyarekebisha. Corder ambaye (keshatajwa) anabaini kuwa makosahujitokeza kwa wingi na si rahisi mwanafunzi kuyatambua. Aidha Selinker na Gass (2008) wanaeleza kuwamakosa yanaweza kutambuliwa tu na mwalimu au mtafiti na wala sio mwanafunzi mwenyewe. Hii ni kwa sababu mwanafunzi hajazielewa kanuni za lugha lengwa.

Corder (1993) anasisitiza kuwa makosani muhimu wakati wa ujifunzaji wa lugha kwa kuwa:

- i) Ni ishara ya mikakati anayotumia mwanafunzi katika kujifunza lugha japokuwa mikakati hiyo si sahihi
- ii) Humjulisha mwalimu kiasi cha lugha ambacho amejifunza mwanafunzi na ni kipi ambacho anahitaji kufunzwa.
- iii) Ni muhimukwa mwanafunzi anayejifunza lugha ya pili kwa kuwa huenda ikawa njia mojawapo au kifaa anachotumia kujifunzia lugha.

2.3.2. Kuteleza

Corder (1967) anabaini kuwakuteleza kwa mwanafunzi hutokana na utendaji na wala sio ishara ya umilisi alionao mwanafunzi. Utendaji kwa mujibu wa Holt (1975) ni jinsi mtu anavyotumia ujuzi wake wa lugha na wala sio ishara ya ujuzi wa lugha alionao. Hii ina maana kuwa mwanafunzi huteleza si kwa sababu hana ujuzi wa lugha bali ni kwa kuwa ameshindwa kutumia ujuzi wake hali ambayo inaweza kusababibishwa na hali yake ya kimwili kwa wakati huo .Kwa sababu hali hii hutokana na utendajihuwa ni rahisi kwa mwanafunzi kujirekebisha binafsi.Kwa mujibu wa Holt (1975), kuteleza hakuna umuhimu wowote katika ujifunzaji wa lugha kwa kuwa ni hali ya kawaida katika matumizi yoyote ya lugha. Corder (ambaye keshatajwa) anaeleza kuwahali ya kutelezahutokana na hali ya mwili wa binadamu kama kusahau, uchovu wa mwili, utelezi wa ulimi au kalamu hali ambayo pia hujitokeza hata kwa wazawa wa lugha wenye umilisi kamili wa lugha yao. Kulingana na Miller (1966) kuteleza hakuna umuhimu wowote katika ujifunzaji wa lugha kwa hivyo hamna haja ya kuuchunguza.

Wanaisimu wengi wanaonekana kuwa na mwelekeo wa kutumia dhana ya umilisi na utendaji ili kutofautisha dhana hizi mbili japokuwa Edge (1996) anarejelea miundo yote

ya lugha inayokiuka miundo sahihi kama kuteleza. Aidha anataja aina tatu za utelezikama zifuatazo:

i)Utelezi ambao kulingana naye hutokea kwa kuwa mwanafunzi hakuwa makini. Aidha mwanafunzi akipewa nafasi ana uwezo wa kujikosoa. Kwa mujibu wa James (1998) utelezi unaweza kuwa wa ulimi mtu anapozungumza au wa kalamu anapoandika.

ii)Makosa kulingana naye James (1998) hutokana na umilisi hivi kwamba, mwanafunzi anafanya makosa kwa kuwa hajakata ujuzi kamili wa lugha lengwa. Hivyo mwanafunzi hawawezi kujikosoa binafsi

iii) Majaribio potovu ambapo mwanafunzi hutumia miundo potovu ili kuwasilisha ujumbe anaotaka.

Japokuwa Brown (2000) anasisitiza kuwa ni sharti makosa na kuteleza kwa mwanafunzi kutofautishwa wakati wa ufunzaji wa lugha ya pili, Corder (1967) anaeleza kuwa ni vigumu kwa mtafiti kutofautisha makosa na kuteleza kwa mwanafunzi. Aidha Freeman na Johnson (1998) wanaeleza kuwa mwanafunzi anaweza kujikosoa anapoteleza lakini ni vigumu kwa mtafiti kutambua anachoweza kujikosoa mwanafunzi. Kwa upande wake Brown (2007) anasema kuwa makosa katika ujifunzaji wa lugha ya pili hutokea kwa kuwa wanafunzi hao hawatambui mfumo na kanuni za lugha husika. Kulingana naye wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili hawana ujuzi wa lugha hiyo kwa hivyo hawawezi kutambua makosa. Kulingana na maelezo yake ni kuwa wanafunzi bado wanajifunza lugha ya Kiswahili hivyo itakuwa vigumu kwao kutambua wanapoteleza. Ni kwa sababu hizi, katika utafiti huu maumbo yote ya maneno yasiyo sahihi yatachukuliwa kama makosa.

2.4. Kiini cha Makosa

Kulingana na Gas, (1979) wanaisimu wa kinadharia na walimu wa lugha wanakubaliana kuwa katika kuwasiliana kwa kutumia lugha ya pili wanafunzi uhamisha vipengelevya lugha yao ya kwanza hadi kwa lugha ya pili. Uhamishaji unaelezwa na Richards (1974b:10) kama matumizi ya vipengele vya lugha fulani wakati mtu anapojifunza lugha nyingine. Aidha, kulingana naye hali hii hupatikana katika viwango tofauti vya lugha kama fonolojia, mofolojia, sintaksia, leksia nahata semantiki. Pia anaeleza sababu tatu za kutokea kwa makosa katika ujifunzaji wa lugha ya pili.

- i) Uhamishaji ambapo mwanafunzi huhamisha vipengele vya lugha yake ya kwanza hadi lugha ya pili yaani athari ya lugha ya kwanza.
- ii) Mikakati ya kujifunza ambayo mwanafunzi hubuni kama ujumlishaji wa sheria za lugha ambapo hutumia sheria za lugha ya kwanza katika lugha ya pili.
- iii) Mbinu ya mwanafunzi ya kutaka kurahisisha kile anachojua ili kusema alichotaka kusema.

Aidha Cook (1992) anasisitiza athari ya L1 kwa L2 anaposema kuwa licha ya juhudi za mwalimu katika kufundisha L2 wanafunzi huwa na ujuzi wa L1 akilini mwao. Hivyo mwanafunzi hutumia ujuzi wa lugha yake ya kwanza kwa lugha ya pili.

Kando na athari ya lugha ya kwanza muktadha wa ujifunzaji wa lugha unaweza kupelekea mwanafunzi anayejifunza lugha ya pili kufanya makosa kwa mujibu wa Brown (2007). Kulingana naye mwalimu au kitabu anachorejelea mwanafunzi kinaweza kumpotosha na kupelekea kufanyika kwa makosa. Makosa ya aina hii Schumann na Stenson (1974) anayarejelea kama ya mtagusano. Hivi kwamba husababishwa na mtagusano wa mwanafunzi na mazingira anamojifunzia lugha. Kwa

upande wake Richards (1974a) anaeleza kuwa wanafunzi hufanya makosa kwa sababu ya kiwango cha chini ambacho mwanafunzi amejifunza lugha. Hii ina maana kuwa mwanafunzi anafanya makosa kwa kuwa kiwango cha lugha ambacho amejifunza bado ni cha chini hivyo hajakata umilisi kamili wa lugha lengwa.

Kwa upande mwingine Selinker na Gass (2008) alibainisha mifanyiko ya kisaikolojia ambayo huchangia kuwepo kwa makosa kama: Kwanza ni kuhamishwa kwa lugha ambapo mwanafunzi huhamisha mfumo wa lugha ya kwanza hadi kwenye mfumo wa lugha ya pili. Hii ni kwa sababu mwanafunzi tayari anajua lugha yake ya kwanza. Iwapo lugha ya kwanza na lugha lengwa hazifanani, basi uhamishaji huo husababisha makosa. Sababu nyingine ya mwanafunzi kufanya makosa ni kutumika kwa mikakati mibaya kufundisha lugha ya pili ambapo mwanafunzi humwelewa mwalimu wake vibaya. Mwanafunzi hujifunza kwa kuiga na hivyo iwapo mwalimu wake atatumia lugha yenye makosa basi mwanafunzi ataiga lugha pamoja na makosa hayo. Sababu ya tatu kwa mujibu wa Selinker ni ujumlashaji mno ambapo mwanafunzi huzijumlisha kanuni za lugha lengwa. Hii inatokana na hali kwamba mwanafunzi anajua kanuni za lugha ya kwanza na apozitumia kwa lugha ya pili basi hufanya makosa. Aidha kanunihizi hujumlishwa iwapo zinakaribiana sana na za lugha ya kwanza. Tano ni mikakati ya kujifunza lugha ya pili ambapo mwanafunzi husahilisha sarufi ya lugha ya pili ili aweze kuwasiliana kwa urahisi zaidi.

2.5. Uainishaji wa Makosa

Makosa katika ujifunzaji wa lugha ya pili yamefanyiwauchunguzi na kuainishwa katika aina mbalimbali. Wanaisimu Dulay (1982) wanarejelea aina moja ya makosa ambayo ni makosa yanayotokana na athari ya lugha ya kwanza. Wakichunguza makosa yanayotokana na athari ya lugha ya kwanza ya wanafunzi wa Kiispania wanapojifunza

lugha ya Kiingereza, Alonso Alonso (1997) waliorodhesha makosa hayo katika makundi matatu kutegemea na idadi ya makosa hayo.

Kwanza makosa yaliyotokana na athari ya fonolojia ya Kiispania. Hii ina maana kuwa sauti za lugha ya Kiispania zilivuruga miundo ya maneno ya lugha ya Kiingereza. Pili ni makosa yaliyotokana na tafsiri ya moja kwa moja kutoka Kiispania hadi Kiingereza. Tatu ni makosa ya ubadilishaji ambapo maneno ya Kiispania yalitumika pale mwanafunzi aliposhindwakupata neno la Kiingereza. Utafiti wake ni muhimu sana kwa kazi hii kwa kuwa kama alivyobaini lugha moja inaathiri nyingine katika kiwango cha kifonolojia na utafiti huu unaangazia athari ya lugha ya Kikamba kwa lugha ya Kiswahili.

Naye Odlin (1989) alifanya utafiti kudhibitisha iwapo fonolojia ndicho kipengele ambacho kingetumika kujua lugha ya kwanza ya mwanafunzi anayejifunza lugha ya pili. Katika utafiti wake alitumia wanafunzi waliozungumza lugha ya Kikorea na Kiispania kama lugha zao za kwanza. Matokeo yake yalibaini kuwa vipengele vingine vya lugha kama sintaksia vingetumika. Kwa upande wake Richards (1974b) alibaini aina mbili za makosa. Makosa yanayotokana na athari ya lugha ya kwanza na makosa yanayotokana na lugha lengwa yenyewe kwa maana kuwa mwanafunzi anafanya makosa haya kwa sababu hajajifunza kikamilifu kanuni za lugha lengwa.

Corder (1974) alibaini kuwa katika kujifunza lugha ya pilimwanafunzi hupitia hatua tatu kabla ya kufikia umilisi kamili wa lugha hiyo. Kila hatua hudhihirisha makosa kwa sababu mahususi. Kulingana naye makosa katika hatua ya kwanza ya ujifunzaji wa lugha hutokea kwa kuwa mwanafunzi hajui mfumo wa lugha ya pili. Makosa katika hatua ya pili hujitokeza kwa kuwa mwanafunzi anatumia vibaya kanuni za lugha ya pili. Katika hatua ya tatu mwanafunzi anafanya makosa kwa nadra na wakati mwingine anaweza

kuyarekebisha yeye binafsi. Kutokana na maelezo ya Corder (1974) inabainika kuwa makosa ya wanafunzi hupungua kadiri anavyoendelea kujifunza lugha.

Kwa upande mwingine Ellis (2008) anajadili mikakati ambayo wanafunzi hutumia katika kujifunza lugha ya pili.

- i) Ufasili ambapo mwanafunzi hujaribu kurahisisha maelezo. Hii ina maana kuwa mwanafunzi hueleza ujumbe wa lugha lengwa kwa kutumia lugha nyepesi ili kuepuka kufanya makosa.
- ii) Udondoshaji wa vipengele vinavyotatiza. Ambapo katika kuandika au kuzungumza mwanafunzi ataviacha vipengele tatizi vya lugha.
- iii) Matumizi ya ishara pale mwanafunzi anapokwama katika kuwasiliana kwa lugha ya pili.

2.6. Misingi ya Nadharia

Imebainika kuwa katika kujifunza lugha wanafunzi hufanya makosa. Corder (1981:36) anaeleza kuwa uelezaji wa makosa ya wanafunzi ni operesheni ambapo makosa huelezwa kwa kutumia nadharia ya kiisimu kwa data iliyokusanywa kwa mwanafunzi au kikundi cha wanafunzi.

Kuna mikabala mitatu ambayo hutumika katika kuchunguza lugha ya wanafunzi katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Mtazamo wa Uchanganuzi Linganuzi, Uchanganuzi Makosa na mtazamo wa Lugha Kadirifu. Mtazamo utakaotumiwa katika utafiti huu ni ule wa Uchanganuzi Makosa. Aidha mitazamo mingine itafafanuliwa kwa kifupi tu.

Kulingana na Lado (1957) nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi hujikita katika ulinganishi wa lugha mbili ili kubaini vipengele vinavyofanana kati ya lugha ya kwanza na lugha ya pili. Misingi wake ni kuwa vipengele vinavyofanana hurahisisha ujifunzaji lakini vipengele vinavyotofautiana hutatiza ujifunzaji wa lugha ya pili. Nadharia hii

haitatumika katika utafiti huu kwa kuwa utafiti huu si linganishi kwa sababu haulinganishi lugha mbili ili kutambua makosa bali unaanza kwa kutambua makosa yenyewe.

Mtazamo wa Lugha Kadirifu uliasisiwa na Selinker (1972). Kulingana naye lugha kadirifu ni lugha iliyo na miundo tofauti na lugha ya kwanza na lugha lengwa. Hii ina maana kuwa lugha hii si mfumo wa lugha ya kwanza au lugha ya pili bali ni mfumo wa kiisimu ambao unajitegemea. Kutokana na maelezo haya tunaelewa kuwa Lugha Kadirifu haichukuliwi kama njia ya ujifunzaji inayoathiriwa na lugha ya kwanza au lugha ya pili. Kwa kuwa utafiti huu unachunguza athari ya kimofonolojia ya lugha ya kwanza kwa miundo ya maneno ya Kiswahili mtazamo huu hautatumika. Hivyo, katika utafiti huu Makosa yatachanganuliwa kwa msingi wa mtazamo wa Uchanganuzi Makosa.

Selinker na Gass, (2008:102) anaeleza kuwa kama lilivyo jina lenyewe Uchanganuzi Makosa ni mtazamo unaojikita katika makosa ya wanafunzi. Aidha Kulingana na Corder (1967), Dulay (1982), Uchanganuzi makosa ni mbinu katika isimu tumikizi inayotumiwa kutambua vipengele vinavyotatiza wanafunzi katika kujifunza lugha ya pili. Isimu tumikizi kwa mujibu wa Selinker na Gass, (2008:102) hurejelea sehemu ya isimu ambayo hutumia nadharia na matokeo ya uchunguzi kwa matatizo ya lugha ikiwemo ujifunzaji wa lugha ya pili. Aidha, Selinker na Gass (2008) Uchanganuzi Makosa hutumiwa katika kuchunguza makosa yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili. Wanaeleza kuwa tofauti na Uchanganuzi Linganuzi ambao hujikita katika kulinganisha lugha ya kwanzana ya pili, Uchanganuzi Makosa huchunguza makosa ya wanafunzi kwa kuzingatia lugha lengwa.

Mwasisi wa mtazamo wa Uchanganuzi Makosa ni Corder (1967) ambaye kupitia makala yake ya *Significance of Learner's errors* nadharia hii ilichukua mwelekeo mpya. Kabla

ya kuchapishwa kwa makala haya, makosa ya wanafunzi yalitazamwa kama kasoro ambazo zilipaswa kuondolewa kabisa lakini Corder alileta mtazamo mpya kwa kusisitiza kuwa makosa yalikuwa muhimu katika ujifunzaji wa lugha. Kulingana na Corder (1974) kutokea kwa makosa katika ujifunzaji wa lugha ni jambo la kawaida na ni muhimu kwa kuwa ni ishara kwamba mwanafunzi anajifunza lugha ya pili na husaidia mwalimu kutathimini mbinu yake ya ufunzaji wa lugha ya pili. Kutokana na maelezo ya Corder ni kuwa makosa ni sehemu muhimu katika ujifunzaji wa lugha. Aidha Corder (1981:25) anasema kuwa Uchanganuzi makosa ni muhimu kwa mwalimu kwa kuwa humwezesha kutathimini mafanikio yake katika kufunza lugha ya pili pamoja na kutambua ni kipi wanafunzi wanahitaji kufundishwa. Pia humwezesha mwalimu kutambua mikakati wanayotumia wanafunzi wake kujifunza lugha ya pili. Richards (1974a) anaeleza umuhimu wa usomaji wa makosa ya wanafunzi.

Kwanza, kujua njia ambazo wanafunzi hutumia kujifunza lugha lengwa.

Pili, kutambua kiini cha makosa na kutambua changamoto katika ujifunzaji wa L2 ili kusaidia mwalimu katika kufundisha L2 pamoja na kuunda vifaa vya kufundishia.

Ellis (2008) anasema kwamba Uchanganuzi Makosa ni muhimu kwa kuwa humpa mtafiti utaratibu wa kuchunguza lugha ya mwanafunzi. Aidha, katika kuchanganua makosa Selinker na Gass (2008), wanapendekeza makosa hayo kuchanganuliwa kupitia hatua zifuatazo.

i) Kukusanya sampuli ya kazi za wanafunzi wanaojifunza lugha lengwa. Katika hatua hii Corder (1974) anapendekeza kukusanywa kwa kazi nyingi ili kuweza kudodoa makosa mengi zaidi. Kulingana naye makosa yanaweza kukusanywa kupitia maandishi au mazungumzo ya wanafunzi.

(ii) Kutambua makosa. Kwa mujibu wa Corder mtafiti anapofikia hatua hii, ni muhimu kwa mtafiti kutofautisha dhana ya makosana hali ya kuteleza. Dhana hizi zimeelezwa katika utafiti huu na kubaini mbinu ya kutambua makosa.

(iii) Kuweka makosa katika makundi. Katika hatua hii kwa mujibu wa Corder makosa yaliyotambuliwa hupangwa katika makundi kulingana na aina yake. Katika kupanga makundi anapendekeza kwamba mtafiti aanze kwa viwango vikubwa vya lugha kama makosa ya mofolojia, sintaksia au msamiati. Makosa katika kila kiwango yanaweza kupangwa katika vikundi hadi vya chini zaidi. Aidha Selinker na Gass (2008:108) kosa moja lisirejelewe kuwa la aina mbili. Kosa liwe la aina A au B.

(iv) Kutathimini kiwango cha makosa katika kila kundi. Hatua hii huhusisha kubaini idadi ya makosa katika kila kundi unaolenga kubaini ni makosa yepi yanayojitokeza zaidi.

(v) Kufafanua chanzo cha makosa. Hatua hii huhusisha kueleza kiini cha makosa. Kwa mujibu wa Corder (1974) hii ndiyo hatua muhimu kati ya hatua zote. Anapendekeza kuwa makosa yaelezwe kwa kuzingatia lugha ya kwanza ya mwanafunzi. Aidha James (1998) anaeleza kuwa katika kueleza kiini cha makosa mtafiti atumie lugha rahisi inayoeleweka kwa uwazi na haraka.

(vi) Kupendekeza njia za kukabiliana na makosa. Hatua hii huhusisha mtafiti kueleza mbinu zinazoweza kutumiwa kukabiliana na makosa.

Aidha Selinker na Gass (2008:104) wanaeleza kuwa umuhimu wa nadharia ya Uchanganuzi makosa ni kuwa kwa msingi wa nadharia hii makosa huchukuliwa kuwa na visababishi vingi, tofauti na Uchanganuzi Linganuzi ambao makosa huchukuliwa kusababishwa na lugha ya kwanza pekee. Hata hivyo, wanasema kuwa udhaifu wa nadharia ya Uchanganuzi Makosa ni kuwahutegemea tu makosa ya mwanafunzi kama

data ya kutathmini iwapo mwanafunzi amejifunza lugha. Kulingana nao mtafiti anafaa kuchunguza vipengele vingine vya lugha ya mwanafunzi ili kupata picha kamili ya lugha hiyo. Pili, wanasema kuwa wakati mwingine ni vigumu kutambua iwapo mwanafunzi amefanyana makosa au ameteleza tu.

Aidha kwa mujibu wa Corder (1967) na Brown (2000) makosa yanaweza kuchunguzwa kulingana na viwango vya lugha. Hii ina maana kuwa tunaweza kuchunguza makosa katika viwango mbalimbali vya kiisimu. Utafiti huu utashughulikia makosa katika kiwango cha kimofonolojia.

2.7.1. Fonolojia

Kulingana na Massamba na wenzake (2004) fonolojia ni tawi la isimu linaloshughulikia uchunguzi, uchambuzi na uanishaji wa sauti pambanuzi ambazo hutumika katika mifumo mbalimbali ya sauti za lugha ya binadamu. Sauti hizi pambanuzi wanazirejelea kama fonimu. Kwa upande mwingine kwa mujibu wa Kamusi ya TUKI (1990), fonolojia ni tawi la isimu ambalo hushughulikia uchambuzi wa mfumo wa sauti zinazotumika katika lugha fulani. Kutokana na maelezo ya wanaisimu hawa inadhihirika kuwa kila lugha ina sauti (fonimu) zake tofauti na nyingine.

Aidha Massamba na wenzake (2004:21) fonimu ni vitamkwa vinavyoweza kujenga maneno yenye maana au vinavyoweza kubadilisha maana za maneno na kuifasili kama kitamkwa kilichobainifu katika lugha fulani maalum. Hii ina maana kuwa kila lugha ina fonimu zake tofauti na lugha zingine. Kwa upande wake Mgullu (1990:57) anaeleza baadhi ya sifa za fonimu kama zifuatazo:

Kila fonimu hushiriki kujenga na kutofautisha maana za maneno

Fonimu moja peke yake haina maana

Ukibadili fonimu katika neno bila shaka maana ya neno hilo itabadilika au kupotea

Ukiongeza fonimu katika neno lolote maana ya neno hilo litabadilika au kupotea

Ukipunguza fonimu au kupangua mpangilio wa fonimu katika neno maana ya neno hili itabadilika au kupotea.

2.7.2. Mofolojia

Katika kufafanua dhana ya mofolojia Posner (1975) anaeleza kuwa mofolojia ni tawi la taaluma ya isimu ambalo huchunguza maumbo ya maneno hususan maumbo ya mofimu naye Hartmann na Stork (1972) anadai kuwa` mofolojia ni tawi la sarufi ambalo hushughulika na uchunguzi na uchambuzi wa maumbo, fani na aina za maneno yalivyosasa pamoja na historia zao. Tukizingatia maelezo haya ni wazi kuwa mofolojia kama tawi la isimu hujishughulisha na maumbo ya maneno.

Booij (2012:8) anataja mofimu kama viungo vya kuundia maneno naye Kamusi ya TUKI (1990) anaeleza mofimu kama kipashio kidogo kabisa amilifu katika maumbo ya maneno. Hii ina maana kuwa maneno huundwa kwa mofimu na kwamba kila mofimu huwa na maana. Aidha kwa mujibu wa Matinde (2012), Massamba na wenzake (2004) maana ya mofimu huwakilisha na mofu. Kama wanavyoeleza Nida (1949), Massamba na wenzake (2004:14) mofu ni umbo la neno ambalo huwakilisha mofimu na ambalo hudhihirika kifonolojia linapotamkwa na kiothografia linapoandikwa. Hii ina maana kuwa mofu ni umbo linaloonekana na mofimu ni dhana dhahania inayowakilishwa na umbo hilo. Aidha mofu moja inaweza kudhihirisha maumbo tofauti ambayo Matinde (2012:100) anayarejelea kama alomofu.

Aidha Holt (1975) anatambua aina mbili za mofimu ambazo ni: Mofimu huru na mofimu funge. Kulingana naye mofimu huru huweza kujisimamia peke yake na kuwa na maana kamili kama neno lakini mofimu funge ni sharti ziambatanishwe na mofimu zingine ili

kuleta maana. Mfano neno mama lina mofimu moja kwa sababu haliwezi kugawa katika vijisehemu vidogo vyenye maana na liiwa peke yake tunaelewa maana yake kikamilifu. Neno mtoto lina mofimu mbili m-toto ambazo kila mojawapo ina maana-m- inawakilisha umoja na –toto- ni mofimu ambayo ni mzizi.

Mzizi kwa mujibu wa Massamba na wenzake (2001) ni kipashio ambacho ndicho kiini cha maneno. Ni maumbo ambayo hayawezi kugawika tena katika sehemu nyingine bila kupoteza uamilifu wake wa kuwa kiini cha maana. Hivyokila mojawapo ya hizi mofimu imeundwa kwa fonimu. Iwapo fonimu hizo zitabadilika basi maumbo ya mofimu yatabadilika. Aidha Holt (1975) anaeleza kuwa baadhi ya mofimu funge huja kabla ya mzizi wa neno na zingine hupatikana baada ya mzizi wa neno. Aidha kwa mujibu wake ni kuwa mofimu funge zinatokana na mifanyiko ya kimofolojia ya unyambuaji na uambishaji. Anaeleza mofimu za unyambuaji kama mofimu ambazo huwekwa kabla au baada ya mzizi na hulenga kuunda neno jipya. Aidha mofimu hizo huweza kubadili kategoria ya kisarufi ya neno. Mfano neno imba lina mofimu mbili imb-a na kategoria yake ya kisarufi ni kitenzi. Neno hili likiongezwa mofimu -wa-kabla ya mzizi na mofimu -ji- baada ya mzizi –imba- tutaunda neno jipya mwimbaji ambalo kategoria yake ya kisarufi ni nomino. Kwa upande mwingine mofimu za uambishaji ni zile mofimu ambazo uongezewa kwenye mzizi wa neno hili kuongeza maana katika neno hilo bila kubadilisha kategoria ya kisarufi ya neno. Mfano, katika neno mtoto m-ni mofimu ya umoja na -toto ni mzizi wa neno. Mofimu wa- ikiwekwa kabla ya mzizi neno hili litakuwa watoto. Katika hali hii neno mtoto litabakia kuwa nomino ila mofimu wa imeongezwa maana ya wingi. Ufafanuzi wa mofolojia na dhana za kimofolojia kama mofu na mofimu ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa mofolojia ni sehemu ya mofofonolojia.

2.7.2.1. Dhana ya Neno

Kama anavyoeleza Holt (1975) kila mzawa wa lugha anajua maneno ya lugha yake na hii ni sehemu mojawapo ya umilisi wa lugha yake. Kulingana naye kujua neno ni kujua sauti zake pamoja na maana yake. Hii ina maana kuwa kila mzungumzaji wa lugha anajua maumbo sahihi ya maneno ya lugha yake kwa kujua sauti zinazounda maneno hayo pamoja na maana yake japokuwa utafiti huu hautajihusisha na maana ya maneno.

Lakini kama anavyoeleza Habwe na Karanja (2004) dhana ya neno ni tata mno hasa katika kubainisha kati ya neno na vipashio vingine katika lugha. Kulingana naye neno ni kipashio cha kiisimu kinachoundwa kwa mofimu moja au zaidi. Kwa upande mwingine Katamba (1993) anaeleza kuwa dhana ya neno inaweza kufafanuliwa kwa misingi mitatu. Misingi ya kwanza ya leksimu ambayo kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004) leksimu ni kipashio kidogo cha msamiati ambacho kina uwezo wa kusimama peke yake kama kidahizo. Kidahizo ni msamiati ambao huorodheshwa katika kamusi.

Misingi ya pili ni kwa kuzingatia muundo wa neno ambao kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004) hurejelea miundo mbalimbali ya leksimu katika tungo au maandishi. Mfano, leksimu lima inaweza zalisha maneno kama limisha na mkulima. Hii ina maana kuwa iwapo tutaeleza dhana ya neno kwa kuzingatia muundo wa neno, lima, limisha na mkulima yatakuwa maneno tofauti. Misingi ya tatu katika kueleza dhana ya neno kwa mujibu wake Katamba (1993) ni kwa kutumia dhana ya neno la kisarufi. Kulingana naye neno linaweza kuwa kiwakilishi cha leksimu kinachohusishwa na sifa za kimofosintaksia kama vile nomino, kitenzi, au kivumishii. Hii ina maana kuwa tunaeleza dhana ya neno kwa kuzingatia kazi ya kisarufi inayotimizwa na neno hilo katika tungo.

Ufafanuzi wa dhana ya neno ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa utachunguza maumbo ya maneno. Aidha mtafiti anazipata fasili za wanaisimu hawa kuhusu dhana ya neno kuwa muhimu kwa kuwa msingi yote mitatu itafaa katika utafiti huu.

2.8. Makosa yanayosababishwa na Athari ya Lugha ya Kwanza

Tafiti mbalimbali zinadhihirisha kuwa kuna athari ya lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Dušková (1969) anabaini kuwa makosa katika ujifunzaji wa L2 yataeleweka kwa kuzingatia L1 ya mwanafunzi. Yeye alifanya utafiti kuhusu makosa ya kileksia yaliyofanywa na wanafunzi wa Czech katika insha zao. Alitambua kuwa wanafunzi walifanya makosa ya tahajia pamoja na kutumia visawe vya maneno visivyofaa. Aidha alibaini kuwa makosa mengi yalitokana na athari ya L1. Utafiti wake utafaidi utafiti kwa kuwa unaangazia jinsi ya kutambua makosa yanayotokana na athari ya lugha ya kwanza.

Kwa upande wake Kattam (2016) alifanya utafiti kubaini iwapo fonolojia ya lugha ya Kinandi ilisababisha makosa ya kimaandishi ya wanafunzi ambapo alibaini kuwa makosa ya tahajia yalitokana na tofauti za kifonolojia katika lugha hizi mbili. Utafiti wake ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa utachunguza makosa katika insha za wanafunzi katika lugha ya Kikamba. Utafiti wake ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa alishughulikia lugha ya Kinandi na utafiti huu ulishughulikia lugha ya Kikamba. Utafiti wake ulimfaidi sana mtafiti kwa kuwa ni kielelezo cha jinsi ya kushughulikia makosa yanayohusiana na athari ya lugha ya kwanza. Pia, katika kuchunguza athari ya lugha ya kwanza katika kazi zilizoandikwa na wanafunzi Macharia (2013) alifanya utafiti kuhusu fonolojia ya lugha ya Kikuyu kama kiini cha makosa na kubaini kuwa makosa ya tahajia yalitokana na fonolojia ya lugha ya kwanza. Kazi za watafiti zilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa ulichunguza makosa katika insha za wanafunzi. Tofauti na utafiti wake ambao ulihusisha lugha ya Kikuyu, utafiti huu utashughulikia lugha ya Kikamba.

Naye Dušková (1969) anabaini kuwa makosa katika ujifunzaji wa L2 yataeleweka kwa kuzingatia L1 ya mwanafunzi. Yeye alifanya utafiti kuhusu makosa ya kileksia yaliyofanywa na wanafunzi wa Czech katika insha zao. Alitambua kuwa wanafunzi walifanya makosa ya tahajia pamoja na kutumia visawe vya maneno visivyofaa. Aidha alibaini kuwa makosa mengi yalitokana na athari ya L1. Maelezo yake yalikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa ulichunguza iwapo lugha ya Kikamba kama L1 inaathiri lugha ya Kiswahili kama L2. Kazi yake ni muhimu kwa kuwa ilimwagazia mtafiti jinsi ya kutambua makosa. Tofauti na utafiti huu alichunguza makosa ya leksia na utafiti huu umechunguza makosa ya kimofonolojia.

Wakizungumzia kiini cha makosa, Littlewood na William (1984), Selinker na Gass (1992) Selinker (1992) na Lado (1957) wanasema kuwa makosa mengi husababishwa na uhamishaji wa miundo ya lugha ya kwanza hadi lugha ya pili. Aidha wanabainisha aina mbili za uhamishaji anazopuzungumzia kuhusu uhamishaji saidizi na uhamishaji potovu. Kulingana nao iwapo L1 na L2 zina miundo inayofanana hali hii itasaidia katika ujifunzaji wa L2 lakini iwapo miundo yake ni tofauti ni sharti L1 kutatiza ujifunzaji wa L2. Aidha ansema kuwa wanafunzi uhamisha miundo na kanuni za L1 kwa L2 bila kukusudia. Maelezo yao yalimfaa mtafiti kwa kumwagazia jinsi ya kushughulikia makosa yanayotokana na athari ya lugha ya kwanza. Kwa mujibu wa Odlin (1989) miundo ya kifonolojia, mofolojia na kisintaksia ya L1 huathiri utoaji wa miundo ya L2 pamoja na matamshi yake. Maelezo yake Lado ni muhimu kwa kazi hii kwa kuwa inachunguza iwapo miundo ya Kikamba inaathiri miundo ya lugha ya Kiswahili.

Musau (1993) alichunguza jinsi wanafunzi wa Kiswahili wanaosomea taaluma ya ualimu wa shule za msingi nchini Kenya wanavyojifunza fonolojia ya Kiswahili sanifu. Katika utafiti wake anadhihirisha kuwa wanafunzi hawa wanaathiriwa na lugha zao za kwanza hasa kwa kubadilisha fonimu za Kiswahili na fonimu za lugha zao za kwanza

zinazokaribiana nazo. Utafiti wake ulihusisha wanafunzi wenye L1 tofauti wa Kikamba, Kimaasai, Kibukusu, Kinandi, Gikuyu, Kisomali na Kidholuo. Utafiti wa Musau ni muhimu sana kwa kuwa ulimwagazia mtafiti namna ya kutambua makosa yanayotokana na athari ya lugha za kwanza hasa lugha ya Kikamba. Tofauti na utafiti huu alishughulikia makosa ya kifonolojia bila kuhusisha mofolojia na utafiti unahusisha viwango vya kifonolojia na mofolojia. Aidha utafiti wake uliangazia vipengele vya kifonolojia kama toni na kiimbo. Tofauti na utafiti huu alitumia nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi na Lugha Kadirifu nao utafiti huu ulitumia nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Aidha utafiti wake haukueleza mikakati ya kukabiliana na makosa ya wanafunzi swala ambalo limeangaziwa katika utafiti huu.

Katika kuchunguza makosa ya kileksia, Mutiga (2002) alitambua kuwa wanafunzi hufanya makosa mengi yakiwemo ya tahajia na utohozi usiofaa. Aidha anaonyesha kuwa makosa hayo yanachangiwa na athari ya lugha ya kwanza. Utafiti wake ni muhimu kwa kazi hii kwa sababu ulimulikia mtafiti namna ya kutambua makosa. Tofauti kati ya utafiti huu na kazi yake ni kuwa alishughulikia lugha ya Gikuyu nao utafiti huu unajihusisha na lugha ya Kikamba. Aidha alichunguza makosa kwa mtazamo wa lugha kadirifu na utafiti huu utatumia mtazamo wa uchanganuzi makosa. Naye Shalaby na wenzake (2009) walifanya utafiti kuhusu makosa ya kileksia katika insha za wanafunzi wa chuo cha Saudi wanapojifunza Kiingereza. Walibaini kuwa wanafunzi wanafanya makosa ya tahajia, na uhamishaji. Aidha kiini cha makosa ya tahajia ni tofauti za kifonolojia zilizopo kati ya L1 ya wanafunzi na lugha ya Kiingereza. Utafiti wao ulimfaa mtafiti kwa kuwa ulimwagazia jinsi ya kuchunguza makosa na kuyaweka katika makundi.

Waweru (2012) alichunguza makosa ya kileksia yanayofanywa na walimu wa shule za chekechea katika mazungumzo yao ya lugha ya Kiingereza. Aliweka makosa hayo katika

makundi ya makosa ya athari ya lugha ya kwanza na makosa ya uhamishaji. Utafiti wake ni muhimu kwa kazi hii kwa sababu unaangazia kuhusivigezo vya kuainisha makosa ya kisemantiki katika makundi kulingana na uhusiano wake. Tofauti na kazi hii alichunguza lugha ya Kiingereza nao utafiti huu unachunguza lugha ya Kiswahili. Aidha katika utafiti wake alitumia mtazamo wa lugha kadirifu nao utafiti huu unatumia mtazamo wa uchanganuzi makosa.

Makosa ya kifonolojia, mofolojia na ya kisintaksia yalifanyiwa uchunguzi na Al-Badawi (2012). Alitafiti wanafunzi wa chuo kikuu cha King Khalid wanapojifunza Kiingereza. Katika utafiti wake alilinganisha lugha ya Punjabi na lugha ya Kiingereza. Alidhihirisha kuwa tofauti za kimuundo kati ya lugha hizi mbili ni kikwazo kwa ujifunzaji wa L2 na ndio husababisha makosa wakati wanafunzi wanapohamisha miundo ya lugha ya Punjabi kwa lugha ya Kiingereza. Utafiti wake ulikuwa na manufaa kwa utafiti huu kwa kuwa ulitoa mwanga wa jinsi ya kushughulikia makosa yanayotokana na athari ya L1. Tofauti na utafiti huu, ni kwamba Kaur aliangazia makosa yanayofanywa na wanafunzi wa chuo kikuu. Utafiti huu unaangazia makosa yanayofanywa na wanafunzi wa shule za upili. Mudhune (1994) katika uchunguzi wake kuhusu matatizo ya kimfosintaksia yanayowakumba wanafunzi wajaluo katika kujifunza Kiswahili kama L2 alibaini kuwa tofauti zilizoko kati ya Kidholuo na Kiswahili ni kikwazo kwa wanafunzi wazungumzaji wa Kidholuo wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Katika uchanganuzi wake alitumia nadharia ya uchanganuzi linganuzi. Utafiti wake unatofautiana na utafiti huu kwa kuwa ulitumia nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Utafiti huu ulishughulikia lugha ya Kikamba ambayo ni tofauti na kidholuo. Pia alishughulikia makosa ya kimfosintaksia na kazi hii ilichunguza makosa ya kimofonolojia. Aidha utafiti wake Mudhune ulimfaidi mtafiti kwa kuwa ulitoa mwanga wa jinsi ya kushughulikia makosa yanayotokana na athari ya L1. N'gan'ga (2002) katika utafiti wake alishughulikia makosa ya kisarufi ya kimofolojia,

kisintaksia na kisemantiki yanayofanywa na wanafunzi wakikuyu wanapojifunza lugha ya Kiingereza. Katika utafiti wake alifafanua kuwa makosa mengi yalitokana na athari ya lugha ya kwanza. Utafiti wake ulimfaidi mtafiti kwa kuwa ulitoa mwanga kuhusu jinsi ya kushughulikia makosa yanayotokana na athari ya lugha ya kwanza. Tofauti na utafiti wake ambao uliangazia lugha ya Kikuyu utafiti huu ulishughulikia lugha ya Kikamba.

Musa (2008) alichunguza athari za lugha ya Kigweno na jinsi zilivyoathiri matokeo ya mtihani wa kidato cha nne. Katika utafiti wake alitumia nadharia ya uchanganuzi Linganuzi. Aidha alishughulikia makosa ya kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Utafiti huu utajishughulisha na makosa ya kimofonolojia. Utafiti wa Musa utamfaidi mtafiti kwa kuwa unamumulikia jinsi ya kuyashughulikia makosa yanayotokana na athari ya L1.

Kazi ya Obara (2014) kuhusu makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia miongoni mwa wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii wanapojifunza Kiswahili inaonyesha kuwa lugha ya Ekegusii inapoingiliana na lugha ya Kiswahili kanuni za sarufi za lugha ya Kiswahili huvurugwa hasa mpangilio wa maneno. Hali hii inatokana na uhamishaji wa kanuni za L1 kwa L2. Aidha utafiti wake unadhihirisha kuwa ijapokuwa lugha ya Ekegusii na lugha ya Kiswahili ni za asili moja zina miundo tofauti. Kazi ya Obara ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu inatoa mwanga kuhusu tofauti zilizopo baina ya Kiswahili na lugha zingine za kibantu. Pia utafiti wake unatoa mwanga kuhusu jinsi ya kuyashughulikia makosa yanayotokana na athari ya L1. Tofauti kati ya utafiti wake na kazi hii ni kuwa alishughulikia lugha ya Ekegusii nao utafiti huu ulishughulikia lugha ya Kikamba.

Kwa upande wake Otiende (2013) alichunguza athari za kimofonolojia za kilosuba katika matumizi ya Kiswahili Sanifu. Katika utafiti wake anaonyesha kuwa silabi hueleza

muundo wa kifonolojia wa neno. Anaonyesha kuwa Kilosuba na Kiswahili zina maneno mengi yanayofanana lakini maneno yenyewe yana muundo tofauti. mfano neno kinu kwa kilosuba ni ekinu. Miundo ya silabi katika maneno haya inasawiana lakini maneno yenyewe ni tofauti. Aidha alibaini kuwa kuna tofauti kati ya fonimu za lugha ya Ekegusii na lugha ya Kiswahili ambazo ndizo chanzo cha makosa ya kifonolojia. Kazi yake Otiende ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa inatoa mwanga wa jinsi ya kuyashughulikia makosa yanayotokana na athari ya L1. Tofauti kati ya kazi ya Otiende na kazi hii ni kuwa alishughulikia lugha ya Kilosuba na utafiti huu unahusu lugha ya Kikamba.

Naye Kanake (2013) alishughulikia makosa ya kifonolojia miongoni mwa wanafunzi wa kiigembe katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Kazi yake ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa inatoa mwanga wa jinsi ya kushughulikia makosa yanayotokana na athari ya lugha ya kwanza. Tofauti kati ya kazi yake na kazi hii ni kuwa alishughulikia makosa katika kiwango cha fonolojia lakini utafiti huu utashughulikia makosa ya kimofonolojia. Aidha katika uchunguzi wake alitumia nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi na utafiti huu utatumia mtazamo wa Uchanganuzi Makosa.

Ntawiyanga (2014) alishughulikia changamoto za kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Muhanga, nchini Rwanda. Katika utafiti wake anaonyesha kuwa changamoto nyingi zinatokana na athari ya L1 ya wanafunzi. Kazi yake ni muhimu kwa kuwa ilimulikia mtafiti namna ya kuyashughulikia makosa yanayotokana na athari ya L1.

Kachipela (2014) alishughulikia athari za sheng katika matokeo ya mtihani wa Kiswahili katika shule za msingi. Katika utafiti wake anaonyesha kuwa kuwepo kwa msamiati wa sheng katika kazi ya wanafunzi kunachukuliwa kama makosa. Utafiti wake ni muhimu

kwa kuwa unatoa mwanga wa jinsi ya kutambua makosa katika kazi za wanafunzi. Tofauti na utafiti huu alishughulikia lugha ya sheng nao utafiti huu umeshughulikia lugha ya Kikamba.

Aidha, Kitsao (2015) alichanganua makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi kutoka wilaya ya Ganze. Katika utafiti wake anadhihirisha kwamba makosa hutokea kwa sababu mbalimbali kama ujumulishaji, kutozingatia kanuni za lugha lengwa pamoja na athari ya L1. Kazi yake ni muhimu sana kwa kuwa inammulikia mtafiti namna ya kuyatambua makosa na jinsi ya kuchanganua makosa hayo kwa nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Katika utafiti wake anatumia nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi na Uchanganuzi Makosa. Tofauti na utafiti huu ambao umeshughulikia lugha ya Kikamba utafiti wake ulishughulikia lugha ya Kigiriyama.

Kutokana na kazi za watafiti hawa ni dhahiri kuwa kuna athari ya lugha ya kwanza kwa lugha ya pili wanayojifunza wanafunzi.

2.8 Mofofonolojia ya lugha ya Kiswahili na Kikamba

2.8.1 Kitangulizi

Sehemu hii imeshughulikia vipengele vya kimofofonolojia ambavyo ni muhimu kwa utafiti huu. Vipengele vilivyoshughulikiwa ni vya kifonolojia na vya kimofolojia ambavyo ndivyo msingi wa ufafanuzi na uchanganuzi wa data. Vipengele hivi ni fonimu na silabi za Kiswahili sanifu na za Kikamba, pamoja na mifanyiko ya kimofofonolojia ya lugha hizi.

2.8.2 Fonimu za Konsonanti za Kiswahili sanifu

Mgullu (1999:69) anaeleza kuwa hadi sasa hakuna uwiano wa idadi kamili ya konsonanti za Kiswahili miongoni mwa wanaisimu. Hali hii imepelekea wanaisimu mbalimbali kuanisha idadi tofauti za konsonanti za Kiswahili. Mathalan Palome (1967) aliorodhesha

konsonanti 24, Massamba na wenzake (2004) waliorodhesha konsonanti 23 na viyeyusho viwili na Mohammed (2011) akaorodhesha 26. Utafiti huu utatumia idadi hii ya 26.

Jedw.2.1 Usawiri wa Konsonanti za Kiswahili kutegemea Mahali pa Kutamkia na Namna ya Kutamka.


| Mahali pa kutamkia | Namna ya Kutamka | | | | | | |
|--------------------|------------------|-----------|-----------------|--------|-----------|----------|-----------|
| | Vipasuo | Vikwamiza | Vizuiwa-kwamiza | Nazali | Kitambaza | Kimadede | Viyeyusho |
| Midomo | P, b | | | m | | | w |
| Midomo-meno | | f, v | | | | | |
| Meno | | θ | | | | | |
| Ufizi | t, d | s, z | | n | l | r | |
| Kaakaa ufizi | | ʃ | ʃ, ʒ | ɲ | | | |
| Kaakaa gumu | | | ɣ | | | | J |
| Kaakaa Laini | k, g | h | | ŋ | | | |
| Glota | | j | | | | | |

2.8.3 Irabu za Lugha ya Kiswahili

Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (2001) na Mohammed (2011) lugha ya kiswahili ina irabu tano. Irabu hizi ni: /a/, /ɛ/, /i/, /ɔ/, /u/. Kama ilivyoielezwa sauti hizi hutamkwa bila kuzuiliwa kwa hewa. Aidha irabu huweza kuainishwa kwa kuzingatia vigezo vya mwinuko wa ulimi na sehemu ya ulimi ya ulimi inayohusika katika kutamka. Kwa kuzingatia sehemu ya ulimi tuna irabu za mbele ambazo ni /ɛ/ na /i/, irabu ya kati /a/ na irabu za nyuma ni /ɔ/ na /u/. Kwa kigezo cha mwinuko wa ulimi tunapata kuwa kuna irabu ya chini /a/, irabu za kati /ɛ/ na /ɔ/, na irabu za juu /i/ na /u/.

Aidha wakati wa kutamka irabu kuna zile ambazo hutamkwa kinywa kikiwa mviringo na zingine kinywa kikiwa kimetandazwa. Hivyo kutokana na kigezo hiki tuna irabu mviringo /ɔ/ na /u/ na irabu tandazi /a/, /ɛ/ na /i/

Mch 2.1 Irabu za Kiswahili kutegemea sehemu ya ulimi na mwinuko wa ulimi



Jedw.2.2 Irabu za Kiswahili

| Sehemu ya ulimi | Mwinuko wa ulimi | | |
|-----------------|------------------|------|-----|
| | Chini | Kati | Juu |
| Mbele | | ε | i |
| Nyuma | | o | u |
| Kati | a | | |

2.8.4. Konsonanti za Lugha ya Kikamba

Konsonanti ni sauti zitamkwazo kwa kuzuiwa kwa mkondo hewa katika sehemu mbalimbali kwa mujibu wa Massamba na wenzake (2004). Lugha ya Kikamba ina konsonanti 19. Hii ni kwa mujibu wa Kitavi (1992) na Musau (1993). Japouuwa Mathooko (2004) anatambua konsonanti mbili zaidi r na Φ ambazo zinatumiwa Kitui magharibi, konsonanti hizi mbili hazitatambuliwa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu utafiti huu unahusu lahaja ya Kimachakos na walasi ya Kitui.

Jedw.2.3 Orodha ya konsonanti za Kikamba

| Kiwakilishi cha IPA | Tahajia | Mifano ya Kikamba | Tafsiri |
|---------------------|---------|-------------------|-----------|
| t | t | ota | uta |
| k | k | kesikɔ | kijiko |
| mb | mb | mbɔsɔ | maharagwe |
| nd | nd | mondo | mtu |
| ŋg | ng | ŋgaŋga | kanga |
| s | s | sua | jua |
| ÷ | v | mbɛ÷ɔ | baridi |
| θ | th | θena | shida |
| nz | nz | nzama | kamati |
| nə | nth | nθe | nchi |
| m | m | mɛkɔ | vitendo |
| n | n | menɔ | uchovu |
| ɲ | ny | ɲɔɲi | ndege |
| ŋ | ng' | ɛŋɔi | punda |
| f | ky | fɔmwa | wiki |
| ndz | ngy | ndza | maskini |
| l | l | sila | hukumu |
| w | w | wea | kazi |
| j | y | yoa | njaa |

Konsonanti za kikamba zinaweza kuainisha kulingana na jinsi na namna ya kutamka

| MAHALI PA KUTAMKA NAMNA YA KUTAMKA | MIDOMONI | MENONI | UFIZI | KAAKAAGUMU | KAAKAALAINI |
|---------------------------------------|----------|--------|-------|------------|-------------|
| VIPASUO | | | t | | k |
| VIPASUO NAZALISHI | mb | | nd | | ŋg |
| VIZUIWA | | | | f | |
| VIZUIWA NAZALISHI | | | | ndz | |
| VIKWAMI-ZO | ÷ | θ | s | | |
| VIKWAMIZO NAZALISHI | m | nə | nz | n | ɲ |
| NASALI | | | l | | |
| VILAINISHO | | | | j | |
| VIYEYUSHO | w | | | | |

Jedw.2. 4 konsonanti za Kikamba (Kielelezo cha Kitavi 1992)

2.8.5 Irabu za Kikamba

Massamba na wenzake (2001) wanaeleza irabu kama sauti ambazo hutamkwa bila kuwepo kizuizi katika mkondo hewa hutokao mapafuni kwenda nje. Kwa upande mwingine, Guthrie (1967) anasema kuwa lugha nyingi za Kibantu huwa na idadi ya fonimu za irabu zipatazo tano au saba. Whiteley na Muli (1962), Ndeti (1972) lugha ya Kikamba ina irabu saba. Irabu hizi ni kama zifuatazo: /a/, /ɛ/, /e/, /i/, /ɔ/, /o/, /u/


Jedw.2.5 Orodho ya Irabu za Kikamba

| Kiwakilishi cha IPA | Tahajia | Maneno ya Kikamba | Tafsiri |
|---------------------|---------|-------------------|----------|
| a | a | kana | mtoto |
| ɛ | e | mosele | mchele |
| e | ĩ | kete | mti |
| i | i | mwini | mwimbaji |
| ɔ | o | iko | jiko |
| o | ũ | motu | unga |
| u | u | leu | chakula |

Vokali za Kikamba huweza kuainishwa kupitia vigezo vya mwinuko na mlalo wa ulimi.

Kulingana na mlalo wa ulimi kuna vokali za juu, za juu kati, kati chini na za chini.

Mch 2.2 Kielezo cha vokali za Kikamba



Jedw.2.6 Vokali za Kikamba kuzingatia mwinuko na mlalo wa ulimi

| Mlalo wa ulimi \ Mwinuko wa ulimi | Mlalo wa ulimi | | |
|-----------------------------------|----------------|----------|-------|
| | Mbele | Katikati | Nyuma |
| Juu | i | | u |
| Kati-juu | e | | o |
| Kati chini | ɛ | | ɔ |
| Chini | | a | |

2.8.6 Muundo wa Silabi za Kiswahili na Kikamba

Utafiti huu ni wa kimofonolojia na kamwe huwezi kwepa kushughulikia miundo ya silabi ya lugha zinazohusika katika utafiti. Hii ni kwa sababu silabi ni kipashio mojawapo

muhimu cha kifonolojia na fonolojia ni sehemu mojawapo ya utafiti huu. Aidha kimofolojia maneno na mofimu hutamkwa kwa mafungu ya silabi.

Dhana ya silabi imeelezwa na wanaisimu mbalimbali. Kwa mujibu wa Crystal (1997) silabi ni kipashio cha kifonolojia ambacho ni kikubwa kuliko fonimu lakini kidogo kuliko neno. Nao Massamba na wenzake (2004) wanaeleza silabi kama kipashio cha kifonolojia kinachohusu matamshi ambacho kwacho sauti za lugha hutamkwa mara moja kama fungu moja linalojitegemea kimatamshi. Fungu hilo linaweza kuwa lina sauti moja peke yake au linaweza kuwa na sauti mbili au zaidi kutegemea muundo wa lugha inayohusika.

2.8.6.1 Silabi za lugha ya Kiswahili

Kama ilivyo na uanishaji wa fonimu za konsonanti za Kiswahili kuna mkinzano miongoni mwa wanaisimu kuhusu idadi kamili ya miundo ya silabi za Kiswahili. Mgullu (1999:69), Massamba na wenzake (2004) walibainisha miundo 7, Habwe na Karanja (2004) wakabainisha miundo 4 huku Mwita (2009) akibainisha miundo 5. Hata hivyo wanaisimu hawa wanakubaliana kuwa kuna miundo minne ya kimsingi ya silabi za Kiswahili kama ifuatayo: I, K, KI na KKI. Aidha Polomé (1967:50) anaeleza kuwa silabi iliyo fupi katika lugha ya Kiswahili huundwa kwa irabu au nazali moja huku silabi ndefu ikiundwa kwa konsonanti moja na vokali au konsonanti zaidi ya moja na vokali. Kwa kuwa si lengo ya utafiti huu kuendeleza mjadala kuhusu idadi ya miundo ya silabi za Kiswahili sanifu, kutokana na miundo mbalimbali wanayoorodhesha wanaisimu hawa tutajadili jumla ya miundo nane

2.8.6.1.1 Muundo wa Irabu pekee (I)

o\$a

u\$a

2.8.6.1.2 Muundo wa Konsonanti na Vokali (KI)

pa\$ka

ba\$ba

Muundo huu wa KI ndio unaopendelewa zaidi na maneno katika lugha ya Kiswahili.

2.8.8.1.3 Muundo wa Konsonanti pekee (K)

Kulingana na Massamba na wenzake (2001) muundo huu ni mojawapo wa miundo iliyotokana na lugha ya Kiswahili kukopa maneno kutoka kwa lugha zingine kama lugha ya Kiingereza.

mwa\$f\$ri\$ka

da\$k\$ta\$ri

2.8.6.1.4 Muundo wa Konsonanti, Konsonanti, Vokali (KKI)

ndo\$a

mba\$li

2.8.6.1.5 Konsonanti, konsonanti, Konsonanti Irabu (KKKI)

Massamba na wenzake (2004) wanaeleza kuwa umbo linapatikana katika baadhi za nomino mkopo.

Spri\$ngi spring.

2.8.6.1.6 Muundo wa nazali pekee (N)

Maumbo ya aina hii huhusisha vitamkwa vya nazali /m/ na /n/

m\$to

n\$ne

2.8.6.1.7 Muundo wa Konsonanti, Kiyeyusho na irabu (KkI)

vye\$o

mpw\$a

2.8.6.1.8 Muundo wa Konsonanti, Konsonanti, Kiyeyusho na Irabu (KKkI)

Muundo huu hutokea kwa nadra sana.

mbwe\$ha

2.8.6.2 Muundo wa Silabi za Kikamba

Lugha ya Kikamba ina muundo wa silabi wazi. Hii ina maana kuwa silabi zote za lugha ya Kikamba huishia kwa irabu na hakuna inayoishia kwa konsonanti. Aidha lugha ya Kikamba hudhihirisha maumbo manne ya silabi ambayo ni I, KI, KKI na II.

2.8.6.2.1 Silabi za Irabu pekee (I)

o\$sa (chukua) mwanzoni mwa neno

na\$u (babu) mwishoni mwa neno

mwe\$etu (msichana) katikati mwa neno

2.8.6.2.2 Silabi za konsonanti na irabu (KI)

Huu ndio muundo ambao hujitokeza kwa wingi katika lugha ya Kikamba.

mo\$te (mti)

mo\$ka (mkewe)

2.8.6.2.3 Silabi za konsonanti, konsonanti na irabu (KKI)

ngo\$a (nguo)

ndi\$o (mwewe)

2.8.6.2.4 Silabi za Irabu na Irabu (II)

e\$ia (maziwa)

Aidha lugha ya Kikamba inadhihirisha kuwa na wakaa mrefu katika baadhi ya maneno japokuwa machache. Mfano

nguu (kobe)

o\$soo (uji)

2.8.8 Kanuni za kimofonolojia za Kiswahili na Kikamba

Kanuni za Kimofonolojia ni zile kanuni ambazo hutawala jinsi fonimu zinavyoathiriana katika mazingira maalum ya kimofolojia. Ufafanuzi wa kanuni hizi ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa inahusisha fonolojia na mofolojia. Tutafafanua kanuni za irabu na za konsonanti ambazo ni muhimu kwa utafiti huu.

2.8.8.1 Kanuni za kimofonolojia za irabu

Hizi ni kanuni zinazohusisha irabu mbili kuathiriana zinapokabiliana. Kama anavyoeleza Polomé (1967:59) maathiriano ya irabu hutokea irabu hizo zinapokabiliana katika mazingira ya karibu au hata mbali.

Udondoshaji

Kanuni hii inahusu kuachwa kwa sauti fulani wakati mofimu mbili zinapokabiliana. Katika lugha ya Kiswahili hali ya udodoshaji hutokea iwapo irabu imetanguliwa na irabu nyingine hasa katika mofimu ya kiambishi cha ngeli na kisha kufuatwa na konsonanti nyingine. Mfanyiko huu hutokea kwa nomino za ngeli ya 1,2 na 3.

| | | |
|-------------|------------|----------|
| Ngeli 1: | umbo ndani | umbo nje |
| | /mu+tu/ | /mtu/ |
| | /mu+huni/ | /mhuni/ |
| Ngeli 2: | /wa+atu/ | /watu/ |
| | /wa+ahuni/ | /wahuni/ |
| Ngeli ya 3: | /mu+ti/ | /mti/ |
| | /mu+lango/ | /mlango/ |

Aidha kwa mujibu wa Kihore (2008) irabu /u/inapokabiliana na irabu inayofanana nayo hubakia kama ilivyo.

| | |
|------------|-----------|
| /mu+undo/ | /muundo/ |
| /mu+umini/ | /muumini/ |
| /mu+umba/ | /muumba/ |

Aidha kama wanavyosema Massamba na wenzake (2001:56) udondoshaji wa sauti zinazohusika ni wa namna mbalimbali na hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Kando na udondoshaji wa irabu /u/ katika lugha ya Kiswahili irabu zingine pia hudondoshwa. Aidha irabu ya kwanza ndiyo hudondoshwa na inayofuatia hubakia. Schane (1973) anaeleza kuwa hali hii hutokea ili kuwepo muundo mwafaka wa silabi kwa kuvunja mfuatano wa irabu.

Irabu / a/ na /e/ zinapokabiliana irabu /a/ hudondoshwa

| | |
|-----------|---------|
| /wa+etu/ | /wetu/ |
| /wa+ema / | / wema/ |
| / a+/e/ → | /e/ |

irabu /a/ kudondoshwa inapokabiliana na irabu inayofanana nayo

| | |
|-------------|-----------|
| /cha+ako/ | / chako/ |
| /cha+angu / | / changu/ |
| /a+/a/ → | /a/ |

Kudondoshwa kwa irabu /i/ inapokabiliana na irabu /o/

| | |
|----------|--------|
| /li+ote/ | /lote/ |
| /i+/o/ → | /o/ |

Kudondoshwa kwa /i/ inapokabiliana na /e/

| | |
|------------|-----------|
| /zi+etu/ | /zetu/ |
| /li+enywe/ | /lenyewe/ |
| / i+/e/ → | / e/ |

Katika lugha ya kikamba irabu ya /a/ ya mofu ya udunishaji hudondoshwa inapokabiliana na irabu inayofanana nayo au inapokabiliana na irabu za kati E na ɔ na hutokea kama E na ɔ mtawalia.

| | | |
|--------------|----------|----------------|
| /ka+ana/ | /kana/ | mtoto |
| /ka+avisi/ | /kavisi/ | mvulana mdogo |
| /a+/a/ → /a/ | | |
| /ka+elitu/ | /kelitu/ | msichana mdogo |
| /a+/e/ → /e/ | | |
| /ka+ou/ | /kou/ | iliyooza |
| /a+/ɔ/ → /ɔ/ | | |

Mvutano wa irabu

Kulingana na Kihore na wenzake (2003) hii ni kanuni ambayo kwayo irabu ya mofimu moja inapokabiliana na irabu ya mofimu nyingine (ya mzizi). Kwa mujibu wao irabu hizo huungana na kuzaa irabu moja tu. Aidha kama anavyoeleza Palome Polomé (1967:59) huu ndio mfanyiko wa irabu ambao hutokea sana. Kulingana naye irabu moja huwa ya chini na nyingine huwa ya juu. Anaeleza kwamba wakati wa mfanyiko huu irabu ya chini huvuta juu na irabu ya juu huvuta chini. Matokeo ya mvutano huu hupelekea irabu zilizovutana kutoweka na badala yake kuzaliwa kwa irabu mpya isiyo ya juu wala chini bali ya kati.

| | |
|------------|----------|
| umbo ndani | umbo nje |
| /wa+ingi / | /wengi/ |
| /wa+izi/ | /wezi/ |

Katika mfano huu ni kwamba irabu ya chini /a/ na irabu ya juu /i/ zimeweza kuzaa irabu ya kati /e/

| | | |
|--------|---|-----------|
| /a/ | + | /i/ → /e/ |
| +chini | | +mbele |
| +juu | | +kati |

Hata hivyo kanuni hii wakati mwingine haifanyi kazi katika baadhi ya maneno.

/wa+i+gizaji / /waigizaji/

/wa+i+mbaji/ /waimbaji/

Iwapo ingefanya kazi maneno haya yangetamkwa kama wegizaji na wembaji mtawalia matamshi mabaya hayakubaliki kabisa kama wanavyoeleza Massamba na wenzake (2004).

Inaelekea kuwa katika lugha ya Kikamba hali hii ya irabu ya chini na juukuvutana na kuzalisha irabu mpya kati hupo jokuwa katika maneno machache mno. Katika uchunguzi wake mtafiti aliweza kupata mfano mmoja tu.

/ma+/iθo/ /me+/θo/ /macho/

Maneno mengi katika lugha ya Kikamba hukosa kudhihirisha mvutano wa irabu kama inavyodhihirika katika mifano hii.

/a+inge/ /a+inge/ wengi

/ke+atu/ / ke+ato/ kiatu

/a+ini/ /a+ini/ waimbaji

Uyeyushaji

Kama anavyosema Mgullu (1999) wataalamu wengine hurejelea mchakato huu kama irabu kuwa nusu irabu. Aidha mchakato huu huhusisha irabu za juu /u/ na /i/ ambazo hubadilika na kuwa /w/ au /j/ zinapofuatiwa na irabu zizisofanana nazo. Irabu /u/ inapofuatiwa na irabu yoyote isiyofanana nayo hugeuka na kuwa /w/ nayo irabu /i/ ikifuatiwa na irabu yoyote isiyofanana nayo hugeuka na kujwa /j/.

/mu+imbaji / /mwimbaji/

/u+imbo/ /wimbo/

/mu+alimu/ /mwalimu/

/mi+anzo/ /mjanzo/


Lugha ya Kikamba hudhihirisha mabadiliko ya aina hii.

| | | |
|----------|---------|----------|
| /mo+ekɔ/ | /mwekɔ/ | mwiko |
| /mo+ini/ | /mwini/ | mwimbaji |
| /mi+aka/ | /mjaka/ | miaka |

Tangamano la irabu

Kanuni hii huhusisha athari ya irabu moja kwenye irabu nyingine kiasi cha kuzifanya irabu hizo zielekee kufanana kabisa au kufanana kiasi katika sifa zake za kimatamshi. Sifa hizi za kimatamshi ni kama sehemu ya ulimi ya kutamkia, mwinuko wa ulimi na hali ya mdomo wakati wa kutamka. Mfanyiko huu hudhihirika hasa katika vitenzi vinaponyambuliwa.

| | | | |
|---------|----------|-----------|-------------|
| kitenzi | kutendea | kutendewa | kutendeshwa |
| Piga | pig-i-a | pig-i-wa | pig-i-shwa |
| pika | pik-i-a | pik-i-wa | pik-i-shwa |
| paka | pak-i-a | pak-i-wa | pak-i-shwa |




Katika mfano huu tunatambua kuwa iwapo kiambishi cha mzizi wa kitenzi ni /i/, /u/ au /a/ viambishi vya kauli ya kutendea, kutendewa na kutendeshwa huwa ni /i/.

Irabu /i/ na irabu /a/ zinasifa zinazofanana kwa kuwa zote ni irabu tandazi.

Mabadiliko mengi ya hali hii pia hudhihirika kwenye vitenzi vyenye kiambishi cha mzizi /e/ na /o/ ambapo kiambishi cha kauli huwa /e/.

| | | | |
|-------|----------|-----------|-------------|
| leta | let-e-a | let-e-wa | let-e-shwa |
| cheza | chez-e-a | chez-e-wa | chez-e-shwa |
| choma | chom-e-a | chom-e-wa | chom-e-shwa |
| ota | ot-e-a | ot-e-wa | ot-e-shwa |



Irabu /e/ na /o/ ni irabu za kati hivi kwamba zinapotamkwa ulimi huiniliwa katikati mwa kinywa.

Aidha lugha ya Kikamba pia hudhihirisha kanuni hii ambapo irabu ya mzizi huonyesha uwiano na irabu ya kiambishi cha mnyambuliko wa vitenzi.

| | | |
|---------|----------|-----------|
| kitenzi | kutendea | kutendewa |
| uwa | uw-e-a | uw-e-wa |
| oka | uk-e-a | uk-e-wa |

Katika mifano hii unapata kuwa iwapo irabu ya mzizi ni /u/ au /o/ irabu ya kauli itakuwa /e/. Irabu /u/, /o/ na /e/ ni irabu za kati.

Mzizi wa kitenzi unapokuwa na irabu /ε/ au /ɔ/ irabu ya kauli itakuwa ni /ε/.

| | | |
|---------|----------|-----------|
| kitenzi | kutendea | kutendewa |
| εka | εk-ε-a | εk-ε-wa |
| semba | semb-ε-a | semb-ε-wa |
| ɔsa | ɔs-ε-a | ɔs-ε-wa |

Irabu/ε / na /ɔ/ ni irabu za kati.

2.8.8.2 Kanuni za kimofonolojia za konsonanti

Usilimisho Pamwe wa Nazali

Kwa mujibu wa Njogu na Wenzake (2006) usilimisho ni hali ambayo sauti huiathiri sauti ya pili hadi zikafanana kwa kiasi. Usilimisho pamwe wa nazali ni usilimisho ambao konsonanti ambayo ni nazali hutamkiwa mahali pamoja na konsonanti inayoifuata Massamba (2011). Kwa upande wake Schane (1973) anaeleza mfanyiko huu kama mkubaliano wa nazali na sauti inayoifuatia zitamkiwe sehemu moja. Aidha kuna aina mbili za usilimisho. Usilimisho wa mbele na usilimisho wa nyuma. Katika usilimisho wa mbele sauti iliyo ya pili huadhiri iliyoitangulia na katika usilimisho wa nyuma sauti ya mbele huathiri sauti inayoifuata. Usilimisho pamwe wa nazali hupo katika Kiswahili na Kikamba. Tazama mifano hii:

| | | | |
|-----------|-----------|---------|-------|
| Kiswahili | /m+bɛ gu/ | /mbegu/ | |
| | /m+buzi/ | /mbuzi/ | |
| | /n+dugu/ | /ndugu/ | |
| | /n+dɔa/ | /ndoa/ | |
| Kikamba | /n+zɔu/ | /nzɔu/ | ndovu |
| | /n+zia/ | /nzia/ | njia |
| | /m+bua/ | /mbua/ | mvua |

Ukaakaishaji

Mgullu (1990) akimnukuu Lass (1984) anadai kuwa ukaakaishaji wa fonimu hutokea wakati ambapo fonimu ziziso za kaakaagumu zinapobadilika na kuwa za kaakaagumu. Hii ni aina ya usimilisho ambapo konsonanti amabayo mwanzoni haikuwa na sifa ya ukaakaa hupata sifa hii kutokana na kufuatiwa na kiyeyusho au irabu. Aidha kulingana na Mgullu ukaakaishaji wa fonimu hutokea wakati ambapo fonimu sisizo vizuiwakwamizi hubadilika na kuwa vizuiwa kwamizwa.

/ki+akula/ /ʃakula/

/ki+umba/ /ʃumba/

/ki+ombo/ /ʃombo/

Hapa tunaona kuwa kwamba kipasuo /k/ cha kakaalaini kimebadilika na kuwa kizuiwa kwamizwa /ʃ/ kutokana na kufuatiwa na irabu.

Lugha ya Kikamba pia hudhihirisha mfanyiko huu. Mfano

/ke+aa/ /kjaa/ kidole

/ke+ɔa/ /kɔja/ chura

/ke+ɔɔ/ /kɔɔ/ choo

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1. Kitangulizi

Kerlinger (1986) anaeleza kuwa, mbinu za utafiti huhusisha mpangilio, muundo au msingi unaomwelekeza mtafiti katika kujibu maswali ya utafiti. Sura hii imefafanua mbinu za utafiti kwa kuzingatia mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, vifaa vya kukusanya datana sampuli ya utafiti.

3.2 Mkabala wa Utafiti

Kwa mujibu wa Kothari (2004:5), kuna mikabala miwili ya utafiti. Mkabala wa kwanza ni wa kitakwimu ambao data yake huwa ya kitakwimu. Mkabala wa kitakwimu hujihusisha zaidi na tafiti zinazohusika na data za kimaabara. Mkabala wa pili ni wa kimaelezo ambao kwa mujibu wake matokeo yake huwasilishwa kwa njia ya maelezo. Aidha Kama anavyoeleza Creswell (2017) utafiti wa kimaelezo huhusika zaidi katika tafiti za sayansi za jamii ambazo kwa kawaida data yake huchanganuliwa na kuwasilishwa kwa kuzingatia zaidi maelezo. Kwa kuwa Kiswahili ni mojawapo ya sayansi za jamii mkabala wa kimaelezo utafaa katika utafiti huu. Aidha Herbert na wengine (1989:116) wanaeleza kuwa utafiti wa kimaelezo hueleza jinsi hali ilivyo bila kubadilishwa. Kulingana nao utafiti wa kimaelezo unaweza kutumiwa kueleza kipengele cha ujifunzaji wa lugha ya pili au mchakato wa kipengele hicho. Utafiti huu unahusu ujifunzaji wa lugha ya pili na unalenga kueleza makosa ya wanafunzi kama yatakavyojihidhihirisha katika kazi zao. Hivyo, ni bayana kuwa mkabala wa kimaelezo utafaa katika utafiti huu hata hivyo mkabala wa kitakwimu utatumika japo kwa kiasi kidogo hasa katika hatua ya nne ya Uchanganuzi Makosa ya kutathimini kiwango cha makosa katika kila kundi.

ya mtafiti kuzipitia insha zilizoandikwa na wanafunzi na makosa yaliyodhihirika katika matamshi baada ya mtafiti kuzisikiza rekodi alizonasa wakati wa usomaji wa insha zilizoandikwa na wanafunzi.

3.5. Sampuli ya Utafiti

Kothari (2004) anafafanua sampuli ya utafiti kama kundi ndogo la watafitiwa ambalo huteuliwa kutoka kwa kundi kubwa ili kumpa mtafiti data ya kufanyia utafiti. Aidha kama anavyoeleza Bryman (2012:25), katika tafiti za kinaelezo mojawapo ya changamoto ni kutambua idadi ya sampuli inayohitajika kukidhi mahitaji ya utafiti. Hata hivyo, Kothari (2004:56) anaeleza kuwa sampuli ya utafiti haifai aidha kuwa kubwa au ndogo sana. Ni kwa sababu hii katika utafiti ulihusisha wanafunzi mia moja kutoka shule nne za upili. Wanafunzi waliohusishwa katika utafiti ni wale wa kidato cha pili na cha tatu. Wanafunzi wa kidato cha pili na cha tatu walichaguliwa kwa kuwa katika kiwango chao wanafaa kuwa wamejifunza kiwango fulani cha lugha. Aidha wanafunzi wa kidato cha kwanza hawakushirikishwa kwa kuwa ni mwaka wao wa kwanza shuleni kwa hivyo wanaendelea kuyazoea mazingira ya shule. Wale wa kidato cha nne waliachwa kwa kuwa wanajitayarisha kwa mtihani wao wa kitaifa hivyo huenda wakakosa muda wa kushiriki katika utafiti huu.

Mtafiti alitumia mbinu ya kinasibu ili kuwateua wanafunzi walioshirikishwa. Mbinu ya kinasibu ilitumika kwa kuwa utafiti ulilenga makosa ya wanafunzi bila kuzingatia umri au jinsia ya wanafunzi. Kwa hivyo mwanafunzi yeyote alifaa kwa utafiti huu. Wanafunzi walihitajika kila mmoja kuchukua kijikaratasi kimoja kati ya vingi vilivyoandikwa “ndio” au “la”. Wanafunzi walioochukua vijikaratasi vilivyoandikwa ‘ndio’ walishirikishwa. Robo ya idadi ya wanafunzi katika kila darasa walishirikishwa.

3.6. Vifaa vya Kukusanyia Data

Kama anavyoeleza Kothari (1986:112) uteuzi wa mbinu na vifaa za kukusanya hutegemea maswala kama aina ya utafiti na maswali ya utafiti, gharama za kukusanya data, wakati uliopo wa kukusanya data na uhalisi wa data inayohitajika. Huu ni utafiti wa kimaelezo. Aidha Kothari (1986:3) anajadili baadhi ya mbinu za kukusanya data zinazohusiana na mkabala wa kimaelezo. Baadhi ya mbinu hizi ni:

- a) Ushuhudiaji ambao kwa mujibu wake ni mbinu ya utafiti ambayo hutumika sana katika kuchunguza tabia za watu. Katika mbinu hii mtafiti hurekodi tabia za watu. Aidha mbinu hii hutumika sana kwa watafitiwa ambao hawawezi kujieleza moja kwa moja. Hii ina maana kuwa katika mbinu hii mtafiti anarekodi mazungumzo ya watafitiwa wanapoendelea na shughuli zao za kawaida. Mbinu hii haikutumika katika utafiti huu kwa sababu data ya kimofonolojia iliyohitajika ilihusisha maumbo ya maneno ambayo hujidhihirisha katika kuadika na matamshi.
- b) Mahojiano ni mbinu ambayo huhusisha maswali ya moja kwa moja kwa watafitiwa na mtafiti. Mahojiano yanaweza kuwa ya ana kwa ana au kupitia simu. Mbinu ya mahojiano haitafaa kwa utafiti huu kwa kuwa unanuiia kukusanya data kuhusu makosa katika mazungumzo na pia maandishi.
- c) Hojaji huhusishwa maswali yaliyochapishwa kwa karatasi ambayo watafitiwa hutakiwa kuyajibu. Mbinu hii haitaumika kwa kuwa mtafiti anakusanya data kuhusu makosa na wala sio maoni ya wanafunzi.

Kwa upande wao Herbert na wenzake (1989) walipendekeza mbinu tatu za kukusanyia data inayohusu makosa ya wanafunzi katika kujifunza lugha ya pili. Mbinu ya kwanza ni mtafiti kuwataka wanafunzi kujibu maswali ya tafsiri kwenye hojaji, ya pili ni ya wanafunzi kupewa mtihani na ya tatu ni wanafunzi kutengewa vipindi watambe hadithi. Mtafiti alitumia mbinu ya pili ambapo wanafunzi walipewa mtihani wa insha. Wanafunzi

waliandika insha juu ya, ‘Siku Iliyafana Sana’. Kwa kuwa hii ni insha ya maelezo iliwapa wanafunzi nafasi nzuri ya kujieleza kwa upana. Kila mwanafunzi alihitajika kuandika insha isiyopungua ukurasa mmoja. Aidha baada ya kuandika insha hizo kila mmoja aliisoma insha yake kwa sauti huku mtafiti akirekodi matamshi yao kwa kutumia simu yake ya mkono. Mtafiti alichagua simu ya mkono kama kifaa cha kurekodi kwa sababu ni kifaa ambacho hukutumia kila siku na hivyo ana uzoefu wa kukitumia. Baadaye mtafiti aliyasikiza matamshi ya wanafunzi aliyorekodi huku akinakili maneno yenye makosa kwenye karatasi.

3.7. Uchanganuzi wa Data

Kwa mujibu wa Kothari (2008) uchanganuzi wa data ni mchakato unaohusisha muhtasari wa data kwa kuiweka kwa mpangilio ambao unamwezesha mtafiti kuafikia malengo yake ya utafiti. Katika utafiti huu data ilichanganuliwa kupitia hatua sita za mtazamo wa Uchanganuzi Makosa kama zilivyopendekezwa na Gass and Selinker (2008).

Kulingana nao hatua ya kwanza ni kukusanya sampuli za kazi za wanafunzi ambapo mtafiti alizikusanywa pamoja insha zilizoandikwa na wanafunzi.

Hatua ya pili kwa mujibu wa nadharia ya Uchanganuzi Makosa ni kutambua makosa. Mtafiti alizipitia insha hizo ili kutambua makosa ya kimofonolojia. Kwa kila kosa litakalotambuliwa chini yake lilipigiwa mstari. Pia mwandishi alisikiza matamshi ya wanafunzi aliyorekodi wakati wa kusoma insha zao. Maneno yaliyodhihirisha makosa mtafiti aliyanakili katika kijitabu chake cha utafiti. Ili kutambua makosa mtafiti alitumia ujuzi wake wa sarufi ya lugha ya Kiswahili. Japokuwa Cook (1992) anaeleza kuwa wazungumzaji wengi wa lugha ya pili ni vigumu kupata umilisi kamili kama wazawa wa lugha hiyo. Ingawaje mtafiti sio mzawa wa lugha ya Kiswahili lakini ana umilisi wa kiwango cha juu katika lugha ya Kiswahili kuwapita wanafunzi katika shule ya upili hasa

ikizingatiwa kwamba tayari ana shahada ya kwanza katika somo la Kiswahili. Aidha Chomsky (1961) alipendekeza kuwa utafiti kuhusu uJifunzaji wa lugha ya pili kufanywa na mzungumzaji wa lugha hiyo.

Hatua ya tatu ilikuwa kuweka makosa katika makundi. Katika hatua hii mtafiti aliyachunguza makosa na yale ambayo yaliyohusiana yaliwekwa katika kundi moja.

Hatua ya nne ilikuwa ni kutathimini kiwango cha makosa katika kila kundi. Katika hatua hii mtafiti alieleza asilimia ya makosa katika kila kikundi ambayo iliwasilishwa kupitia mchoro wa grafu.

Hatua ya tano ilikuwa kueleza chanzo cha makosa ambapo mtafiti alichunguza kwa makini mofofonolojia ya lugha ya Kikamba kubaini iwapo ilisababisha kuwepo kwa maumbo potovu ya maneno ya Kiswahili. Hii ni kufuatia mapendekezo yake James (1998) kuwa makosa ya wanafunzi yaelezwe kwa kutumia mfumo fulani wa lugha kwa kuwa Uchanganuzi Makosa hulenga lugha lengwa.

Hatua ya mwisho ilikuwa ni kupendekeza mbinu za kukabiliana na makosa hayo. Katika hatua hii mtafiti alipendekeza mbinu ambazo zingeweza kutumika kukabiliana na makosa ya wanafunzi.

3.8. Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Maneno yaliyodhihirisha makosa ya kimofonolojia yalibainisha na maumbo sahihi kutolewa. Aidha sababu za kutokea kwa makosa hayo zilielezwa na njia za kutatua makosa hayo kupendekezwa. Aidha ili kurahisisha uwasilishaji na uelewaji wa matokeo mtafiti alitumia majwedwali, michoro na vielelezo vilipohitajika.

3.9. Maadili ya Utafiti

Cresswell (2013) akimrejelea Punch na Oancea (2014) anaeleza kuwa mchakato wa utafiti hushirikisha ukusanyaji wa data. Kulingana naye data za utafiti hukusanywa kutoka kwa binadamu na huwa ni habari zinazomhusu binadamu hivyo ni sharti mtafiti kuzingatia maadili wakati wa utafiti. Baadhi ya maadili anayotaja ni mtafiti kupata cheti cha kumruhusu kufanya utafiti kabla ya kwenda nyanjani, kupata idhini kutoka kwa watafitiwa pamoja na kulinda habari za kibinafsi za watafitiwa. Mtafiti alizingatia maadili haya kwa kupata cheti cha kufanya utafiti kutoka chuo kikuu cha Pwani kabla ya kwenda nyanjani, kisha kuomba ruhusa kwa walimu wakuu wa shule alizofanyia utafiti ili kuwaruhusu wanafunzi wao kushiriki katika utafiti. Aidha mafiti aliwaeleza wanafunzi lengo lake la kuwashirikisha katika utafiti.

SURA YA NNE

UCHANGANUZI WA DATA NA MATOKEO

4.1 Kitangulizi

Sura hii ni sehemu ya uchanganuzi wa data ambao unalenga kujibu maswali ya utafiti. Madhumuni ni kutambua makosa ya kimofonolojia, kueleza kiini cha makosa hayopamoja na kupendekeza mbinu za kukabiliana nayo. Uchanganuzi huu wa data uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Makosa kwa kuzingatia hatua zilizopendekezwa na Corder (1960).

Ili kutambua makosa, mtafiti alizikusanya insha zilizoandikwa na wanafunzi akazipitia. Aidha mtafiti alisikiza matamshi ya wanafunzi aliyorekodi na kunakili maneno yaliyodhihirisha makosa. Ili kutambua makosa ya wanafunzi, mtafiti alitumia umilisi wake wa lugha ya Kiswahili ambapo alilinganisha miundoya lugha ya mwanafunzi na miundo sahihi ya lugha ya Kiswahili Sanifu. Aidha, kwa mujibu wa nadharia ya Uchanganuzi Makosa hatua ya pili katika kuchanganua makosa ni kuyaweka makosa yaliyotambuliwa katika makundi. Na kama anavyoeleza Waweru (2012) akimrejelea Norrish (1987), kuna mbinu mbili za kupanga makosa katika makundi. Mbinu ya kwanza ni mtafiti kuunda makundi yake ya makosa kabla ya kutambua makosa, na baadaye kuyapanga makosa katika makundi hayo na njia ya pili ni mtafiti kutambua makosa kwanza na kisha kuunda makundi kutokana na makosa yaliyotambuliwa. Katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu ya pili. Mtafiti aliainisha makosa yaliyotambuliwa katika makundi matatu yafuatay;

Makosa ya uchopekaji

Makosa ya udodoshaji

Matumizi ya sauti mbadala

4.2. Makosa ya uchopekaji

Katika utafiti huu, uchopekaji ni kuongeza kipengele cha kimofonolojia sehemu ambapo hakistahili kuwa.

4.2.1. Uchopekaji wa /u/

Katika lugha ya Kiswahili, kiambishi awali cha kuwakilisha umoja ni {m} katika baadhi ya nomino za ngeli ya 1 na 3. Baadhi ya wanafunzi wa Kikamba walichopeka irabu /u/ kwenye kiambishi hiki na kupelekea kupatikana muundo usio sahihi {mu}. Uchopekaji huu pia ulijitokeza katika baadhi ya viambishi vya nafsi kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.

| umbo lisilo sahihi | umbo sahihi |
|---------------------------|--------------------|
| mutoni | mtoni |
| musimu | msimu |
| mutoto | mto |
| mumoja | mmoja |

Sababu ya kutokea kwa kosa hili ni tofauti za kimofonolojia kati ya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kikamba. Katika lugha ya Kiswahili irabu, /u/ ya kiambishi hudondoshwa katika ngeli ya 1 na 3; mfano katika neno *mtu* lakini katika lugha ya Kikamba kiambishi hubakia kuwa na sauti hiyo kama vile katika neno la Kikamba *mondo* kwa maana ya *mtu*. Wanafunzi wa Kikamba wanafanya makosa kuhamisha muundo huu katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi huchopeka irabu /u/ ili kuunda muundo wa silabi pendwa wa KI na pia kuweza kurahisisha matamshi kwa kuvunja mfuatano wa konsonanti mbili.

4.2.2 Uchopekaji wa irabu /i/

Katika kuandika baadhi ya maneno ya Kiswahili wanafunzi walichopeka irabu /i/ katikati mwa konsonanti. Tazama mifano hii

| umbo lisilo sahihi | umbo sahihi |
|--------------------|-------------|
| pilika pilika | pilka pilka |
| hisitoria | historia |
| alufajiri | alfajiri |
| musitarehe | mstarehe |
| nije | nje |

Makosa haya yalitokana na tofauti kati ya miundo ya silabi ya Kiswahili na Kikamba. Katika lugha ya Kikamba muundo wa silabi ya konsonanti pekee na silabi funge haupo lakini katika lugha ya Kiswahili muundo huu hupatikana aghalabu katika maneno ya mkopo tofauti na lugha ya Kikamba ambapo maneno hukopwa kwa kuzingatia muundo wa lugha ya Kikamba. Mwanafunzi ameandika \$ni\$je\$ badala ya \$n\$je\$. Katika Kiswahili sanifu silabi \$n\$ haina irabu. Mwanafunzi ameiongeza silabi hiyo irabu /i/ kwa kuwa katika lugha yake hakuna maneno yenye muundo wa silabi wa Konsonanti pekee au silabi funge. Pia huchopekaji huu wa irabu umetokana na hali kuwa mwanafunzi alitaka kuvunja mfuatano wa konsonanti na hivyo kuweza kurahisha matamshi kwa kupata muundo pendwa wa silabi ya KI.

4.2.3 Uchopekaji wa /h/

Wanafunzi walichopeka fonimu /h/ katika baadhi ya maneno na katika mofu za viambishi vya nafsi na ngeli, hali iliyopelekea kuwepo kwa miundo isiyo sahihi ya lugha ya Kiswahili.

| umbo lisilo sahihi | umbo sahihi |
|---------------------------|--------------------|
| hakiwa | akiwa |
| hatatupeleka | atatupeleka |
| hilikuwa | ilikuwa |
| hukafika | ukafika |
| sitahisahau | sitaisahau |
| hili | ili |
| hana | ana |
| haste haste | asteaste |
| hulianza | ulianza |
| hudodokwe | udondokwe |
| hadimu | adimu |
| hawe | awe |

Kutokana na mifano iliyotolewa hapa mofu ya kiambishi cha nafsi katika kitenzi *akiwa* ni {a}. Hivyo basi, mwanafunzi alifanya makosa kuchopeka /h/ ambayo ilipelekea kuwepo kwa umbo lisilo sahihi /ha/. Sababu ya wanafunzi kufanya kosa hili ni kwa kuwa lugha ya Kikamba haina fonimu /h/; na kwa sababu hii, baadhi ya wazungumzaji wa Kikamba huichopeka fonimu hii pasipositahili kwa kukosa kujua ni wapi inafaa kutumiwa

4.2.4. Uchopekaji wa {ma}

Wanafunzi walichopeka mofu funge ya wingi {ma} katika baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili na kupelekea kuwepo kwa maumbo yasiyo sahihi ya maneno ya lugha ya Kiswahili kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

| umbo lisilo sahihi | umbo sahihi |
|---------------------------|--------------------|
| mashule | shule |
| mashida | shida |
| mambuga | mbuga |
| madada | dada |

Kiini cha kutokea kwa makosa haya ni tofauti ya miundo ya maneno ya Kiswahili na Kikamba. Katika lugha ya Kiswahili (sanifu) maneno haya hupatikana katika ngeli 9 na 10 ambayo huendelezwa sawa katika hali ya umoja na wingi pasipo kuchukua viambishi vya wingi. Hivyo kuambatanisha mofu {ma} katika maneno haya kunasababisha kuwepo kwa maumbo ya maneno yasiyofaa ni makosa. Maneno yanayochukua mofu *ma* ya wingi ni maneno ya ngeli ya 5. Mfano jiwe na mawe. Katika lugha ya Kikamba maneno haya huchukua kiambishi cha wingi {ma} Mfano ni neno *sukulu* kwa maana ya shule; wingi wake ni *masukulu* yaani mashule.

4.3. Udondoshaji wa /h/

Lugha ya Kikamba inaathiri lugha ya Kiswahili kwa upande wa mofu ya kukanusha na mofu ya mazoea. Katika lugha ya Kiswahili, vitenzi huainisha hali ya mazoea kwa kutumia mofu {hu}. Fonimu /h/ pia hutumiwa katika kiambishi kikanushi {ha} cha nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili umoja na vile vile, wingi na nafsi ya tatu umoja na wingi. Hivyo kudondoshwa kwa /h/ kunafanya mofu hizi kubadilisha umbo pamoja na kupoteza maana, kama inavyodhihirika katika mifano iliyopo hapa chini. Pia maneno mengine ya Kiswahili ambayo huwa na fonimu hii, ilidondoshwa.

| umbo lisilo sahihi | umbo sahihi |
|---------------------------|--------------------|
| uonekana | huonekana |
| ukosa | hukosa |
| aukupita | haukupita |
| atukutaka | hatukutaka |
| ulia | hulia |
| amsahau | hamsahau |
| umo | humo |
| akika | hakika |
| Paali | Pahali |

Sababu ya kutokea kwa hali hii ni kuwa mfumo wa kifonolojia wa lugha ya Kikamba hauna fonimu /h/. Pia katika lugha ya Kikamba, tofauti na sauti nyingine, fonimu /h/ haina sauti nyingine inayokaribiana nayo hivyo wanafunzi wanapokumbana nayo; huidondosha kabisa katika baadhi ya maneno na kupelekea kuwepo kwa makosa wanapoandika au kutamka maneno ya Kiswahili yenye fonimu hiyo.

4.3. Matumizi ya sauti mbadala

Matumizi ya sauti mbadala huhusisha ubadilishaji wa sauti ambapo katika lugha sauti isiyopatikana katika mfumo wake wa kifonolojia huondolewa na badala yake kukatumika sauti nyingine ambayo ni tofauti, lakini inakaribia kufanana na sauti iliyoondolewa.

4.3.1 Matumizi ya /l/ badala ya /r/

Katika baadhi ya maneno ya Kiswahili ambayo katika muundo wake yana sauti /r/, badala yake wanafunzi wa Kikamba walipokabiliana na maneno hayo wao walitumia sauti /l/ walipoandika na hata katika kutamka.

| umbo lisilo sahihi | umbo sahihi |
|---------------------------|--------------------|
| walindi | waridi |
| linda | rinda |
| tunamelemeta | tunameremeta |

4.3.2 Matumizi ya /mb/ badala ya /b/

Wanafunzi wa Kikambakatikakuandika na kutamka, ilibainika kuwa maneno ambayo yalikuwa na fonimu / b/, wanafunzi waliambatanisha fonimu hiyo na fonimu /m/ na kuzua miundo isiyokubalika kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

| umbo lisilo sahihi | umbo sahihi |
|---------------------------|--------------------|
| wamembembwa | wamebebwa |
| Sembuleni | sebule |
| sako kwa mbako | bako |
| sumbira | subira |
| mbamba | baba |
| mkomba | mkoba |
| mbasi | basi |
| mbana | bana |

Sababu ya kutokea kwa makosa haya ni kuwa lugha ya Kiswahili ina fonimu /b/. Tofauti na lugha ya Kikamba ambayo haina foni mu hii. Lugha ya Kikamba ina fonimu /mb/. Hivyo mwanafunzi wa Kikamba alipokabiliwa na maneno yenye fonimu /b/ badala yake alitumia /mb/ ambayo ameizoea katika lugha yake ya Kikamba.

4.3.3 Matumizi ya /nd/ badala ya /d/

Maneno ya Kiswahili ambayo yana fonimu /d/ mwanafunzi mwenye asili ya lugha ya Kikamba huwa badala ya /d/ anatumia /nd/.

| umbo lisilo sahihi | umbo sahihi |
|---------------------------|--------------------|
| kinaga ubanga | kinaga ubaga |
| kukonga | kukoga |
| jongoo | jogoo |

Sababu ya wanafunzi kufanya kosa hili ni kwa kuwa mfumo wa kifonolojia wa lugha ya Kikamba hauna fonimu /d/, ambayo hupatikana katika mfumo wa kifonolojia wa lugha ya Kiswahili, hivyo mwanafunzi alipokabiliwa na maneno yenye fonimu hiyo, badala yake alitumia fonimu inayokaribiana nayo /nd/ ambayo hupatikana katika lugha ya Kikamba; hali ialiyo pelekea kuwepo kwa miundo potovu ya baadhi ya maneno ya Kiswahili.

4.3.4 Matumizi ya /s/ badala ya /z/

Katika baadhi ya maneno ya Kiswahili yenye fonimu /z/ mwanafunzi alitumia fonimu mbadala ya /s/ kama inavyodhihirika katika mifano hii.

| umbo lisilo sahihi | umbo sahihi |
|---------------------------|--------------------|
| hasemeseki | hasemezeki |
| saidi | zaidi |
| wasasi | wazazi |

Lugha ya Kikamba haina fonimu /z/ badala yake ina fonimu /s/. Mwanafunzi wa Kikamba ambaye amezoea kuitumia fonimu /s/ katika lugha yake, huathirika visivyo kuitumia badala ya fonimu /z/ ya Kiswahili.

4.4 Kutathimini kiwango cha makosa yaliyotambuliwa

Kwa mujibu wa nadharia ya Uchanganuzi Makosa, baada ya makosa kuwekwa katika makundi na kuelezwa, hatua yenye kufuata ni kutathimini kiwango cha makosa katika kila kundi. Kwa hivyo, makosa yaliyotambuliwa yaliwekwa katika makundi matano na idadi ya makosa katika kila kikundi ilibainishwa.

Jedw.4. 1 Makundi na kiwango cha makosa

| Aina ya makosa ya kimofonolojia | Uchopekaji | Matumizi ya sauti mbadala | Udondoshaji | Jumla |
|--|-------------------|----------------------------------|--------------------|--------------|
| Jumla ya makosa katika kundi | 171 | 84 | 75 | 330 |
| Asilimia ya makosa katika kila kundi | 51.80 | 25.45 | 22.72 | 100 |

Matokeo haya yanabaini wazi kuwa makosa mengi ya kimofonolojia yalikuwa ya uchopekaji. Uchopekaji huu ulikuwa wa irabu hasa irabu /u/ na irabu /i/. Hii ni kwa

sababu uchopekaji huu una chanzo katika tofauti za miundo ya kimofolojia ya maneno ya Kiswahili na Kikamba na pia tofauti za kifonolojia kati ya lugha hizo mbili. Mathalan, Uchopekaji wa irabu /u/ katika baadhi ya nomino za Kiswahili ni kutokana na sababu kwamba nomino za Kikamba huchukua kiambishi {mu} na katika lugha ya Kiswahili kiambishi cha umoja ni {m}. Aidha kuna sababu za kifonolojia zinazochangia hali hii. Mfumo wa silabi za Kikamba hauna muundo wa silabi funge tofauti na lugha ya Kiswahili ambayo hukubali muundo huu wa silabi. Hivyo wanafunzi wanachopeka irabu /u/ na /i/ ili kuvunja mfuatano wa konsonanti mbili. Kundi la pili lilihusu matumizi ya sauti mbadala ambayo yalichukua asilimia ya 25.45 kuwepo kwa makosa haya kwa wingi kunatokana na tofauti kati ya mfumo wa kifonolojia kati ya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kikamba ambapo fonimu zizizopatikana katika lugha ya Kiswahili badala yake wanafunzi walitumia fonimu za Kikamba ambazo zilikaribia kufanana na zile za Kiswahili. Kwa mfano /l/ badala ya /r/, /mb/ badala ya /b/, /s/ badala ya /z/ na /nd/ badala ya /d/. Kundi la mwisho lilikuwa ni makosa ya udondoshaji ambao ulijitokeza katika matumizi ya fonimu /h/ peke yake.

4.5 Njia za kukabiliana na makosa yaliyotambuliwa katika utafiti

Kwa mujibu wa nadharia ya Uchanganuzi Makosa iliyotumika katika utafiti huu, baada ya mtafiti kutambua makosa ya mwanafunzi ni sharti apendekeze njia za kukabiliana na makosa hayo. Hivyo, mtafiti anapendekeza mbinu zifuatazo zitumike ili kukabiliana na makosa ya wanafunzi.

Kwanza walimu wanaofundisha lugha ya Kiswahili wanafaa kuwa waangalifu wanapokuwa darasani ili wasifanye makosa wanapoandika au kuzungumza. Hii ni kwa sababu mwanafunzi hujifunza lugha kwa kumuiga mwalimu wake na iwapo mwalimu atafanya makosa basi wanafunzi watamuiga na kutamka kama atamkavyo yeye na baadaye kuyahamisha matamshi hayo katika maandishi yake. Ni muhimu sanawalimu

walioathirika na L1 yao kuwa makini wanapokuwa wakifundisha ili kuepuka kufanya makosa wao wenyewe.

Pili, walimu wanaofundisha lugha ya Kiswahili wanafaa wawe na ujuzi wa hali ya juu wa lugha ya Kiswahili, ili wanafunzi wao waweze kujifunza vyema na kuwa kielelezo kwao. Njia nyingine ya kukabiliana na makosa ya wanafunzi ni kuwa walimu wanafaa kuwakosoa wanafunzi wao pindi tu makosa yanapofanyika. Na kuhusu wanafunzi ambao wanafanya makosa wakiwa darasani, mwalimu anafaa kuyakosoa papo hapo. Kuhusiana na Makosa yanayotokea katika mtihani, mwalimu anapaswa ayarekebishe papo hapo na kusisitiza urekebishaji huu darasani ili yasirudiwe na wanafunzi wengine.

Brooks (1968) anasema kuwa njia muhimu ya kuepukana na makosa hayo ni kuwepo kwa mbinu mwafaka za kufundishia pamoja na vifaa. Naye Fries (1945), anatilia mkazo maelezo ya Brooks anaposema kuwa vifaa bora zaidi vya kufundishia L2 ni vile vitakavyoafikiwa baada ya kuchunguza L1 na L2 ya wanafunzi. Hivyo washikadau wa elimu, hasa waandalizi wa mitalaa watoe miongozo ya mbinu za kufundishia ambazo zitawasaidia walimu kuwaelekeza vyema wanafunzi wao ili kuwasaidia ipasavyo kuepukana na makosa. Aidha vifaa vya kufundishia vinavyopendekezwa katika mitalaa viweze kusaidia wanafunzi na walimu wao kuepukana na makosa.

Walimu wanaofunza Kiswahili ni sharti wawe makini na kufahamu kuwa mwanafunzi ana miundo yake ya L1 akilini mwake. Hivyo mwalimu achunguze ni vipengele vipi vya L2 vinavyofanana na vya L1 ya mwanafunzi ili amwelekeze namna anavyoweza kuvitumia kusaidia ujifunzaji wake wa L2. Inafaa mwalimu pia achunguze ni vipengele vipi vya L1 ya mwanafunzi vinavyoweza kumtatiza katika kujifunza L2 na kumwelekeza vilivyo ili aepukane na utataa huo.

Mtagusano kati ya mwalimu na mwanafunzi ni muhimu katika ufunzaji na ujifunzaji wa L2. Japokuwa mwanafunzi anaweza kujifunza lugha hata anapokuwa peke yake, kuwepo kwa mwalimu ni muhimu sana kwa kuwa mwalimu atayarekekebishia makosa pindi tu yanapotokea. Katika shule za upili, kipindi kimoja cha somo la Kiswahili huchukua dakika arobaini peke yake. Katika kipindi hiki, mwalimu anahitajika kuendeleza silabasi. Hivyo hakuna muda mwingi wa mwalimu kuingiliana vilivyo na wanafunzi. Wanafunzi wanakosa nafasi za kujieleza na hata kukosolewa na mwalimu wao. Hivyo kuna haja ya somo la Kiswahili kutengewa muda zaidi na washikadau.

Wanafunzi Wakamba wanafaa kufanya mazoezi mengi katika lugha ya Kiswahili kwa kuandika insha nyingi iwezekanavyo. Kwa kuandika wataweza kupata mazoea ya vipengele vinavyowatatiza na hivyo kupunguza makosa kimofonolojia kati ya lugha ya Kiswahili na ile ya Kikamba. Kwa kufanya hivi wataweza kupunguza makosa haya katika kazi zao.

Wanafunzi Wakamba waandae mijadala mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili ili waweze kukuza stadi yao ya kuzungumza. Kwa kufanya hivi watazoa matamshi sahihi ya maneno ya lugha ya Kiswahili hali ambayo itawasaidia kupunguza makosa.

Aidha wanafunzi wawe makini darasani ili waweze kujifunza kutoka kwa walimu wao wanapoandika na kuzungumza ili waweze kupata miundo sahihi ya maneno ya lugha ya Kiswahili.

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Kitangulizi

Sura hii ni hitimisho ni la utafiti huu na inaangazia, kwa kifupi, matokeo ya utafiti pamoja na mapendekezo ya mtafiti. Sehemu hii inaangazia kuwepo kwa makosa ya kimofonolojia miongoni mwa wanafunzi wa Kikamba wanaojifunza lugha ya Kiswahili, ambayo yanatokana na tofauti za kimofonolojia kati ya lugha hizi mbili. Pia katika sura hii mtafiti ametoa mapendekezo kutokana na utafiti wake na pia akapendekeza tafiti nyingine za baadaye za kuuendeleza utafiti huu zifanywe ikiwezekana.

5.2 Hitimisho

Utafiti huu ulihusu uchanganuzi wa makosa ya kimofonolojia miongoni mwa wanafunzi wenye aslili ya Kikamba wanaojifunza lugha ya Kiswahili kwa kuongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Aidha utafiti huu ulikuwa na malengo matatu. Kwanza kubaini makosa ya kimofonolojia yanayofanywa na wanafunzi Wakamba wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Pili kubaini chanzo cha makosa hayo na tatu ni kupendekeza njia za kukabiliana na makosa hayo.

Uchunguzi wa mtafiti ulibaini kuwa wanafunzi wa Kikamba walifanya makosa ya kimofonolojia walipojifunza lugha ya Kiswahili. Makosa hayo mtafiti aliyaweka kwenye makundi kwa mujibu wa nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Kundi la kwanza lilikuwa ni makosa ya uchopekaji, ambapo wanafunzi walichopeka vipengele vya kimofonolojia sehemu ambapo hazitakiwi kuwa. Mtafiti alitambua kuwa wanafunzi wengi waliichopeka irabu /u/ kwenye kiambishi awali cha kuwakilisha umoja {m} na kupelekea kupatikana muundo usio sahihi {mu} katika baadhiya nomino za ngeli ya 1 na

ya 3 ambazo zina kiambishi awali cha kuwakilisha umoja {m}. Mfano neno *mtoni* wanafunzi walichopeka irabu /u/ na kuwa *mutoni*, na kuibuka na *musimu* badala *msimu*. Aidha mtafiti alibaini kuwa makosa haya yalitokana na tofauti za kimofonolojia kati ya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kikamba. Katika lugha ya Kiswahili irabu /u/ ya kiambishi hudondoshwa katika ngeli ya 1 na 3 mfano katika neno *mtu*, lakini katika lugha ya Kikamba kiambishi hubakia kuwa na sauti hiyo kama vile katika neno la Kikamba *mondo*, kwa maana ya mtu. Aidha ilibainika kuwa wanafunzi walichopeka irabu /u/ ili kuunda muundo wa silabi pendwa wa KI na pia kuweza kurahisisha matamshi kwa kuvunja mfuatano wa konsonanti mbili.

Makosa mengine ya uchopekaji yalikuwa katika matumizi ya konsonanti /h/ ambapo wanafunzi walichopeka fonimu /h/ katika baadhi ya maneno na katika mofu za viambishi vya nafsi na ngeli, hali iliyopelekea kuwepo kwa miundo isiyo sahihi ya lugha ya Kiswahili. Mathalan mofu ya kiambishi cha nafsi katika kitenzi *akiwa* ni {a}. Hata hivyo mwanafunzi alifanya makosa kwa kuchopeka /h/ ambayo ilipelekea kuwepo kwa umbo lisilo sahihi, /ha/. Utafiti ulibaini kuwa sababu ya wanafunzi kufanya kosa hili ni kwa kuwa lugha ya Kikamba haina fonimu /h/, na kwa sababu hii, baadhi ya wazungumzaji wa Kikamba huichopeka fonimu hii pasipostahili kwa kukosa kujua ni wapi inafaa kutumiwa.

Pia makosa mengine ya uchopekaji yaliyogunduliwa ni uchopekaji wa mofu funge ya wingi {ma} katika baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili ya ngeli 9 na 10 ambayo huendelezwa sawa katika hali ya umoja na wingi pasipo kuchukua viambishi vya wingi. Katika lugha ya Kikamba maneno haya huchukua kiambishi cha wingi {ma}. Mfano mzuri ni neno *shule* ambalo wanafunzi waliliambatanisha na mofu ya wingi na kuwa *mashule*. Katika lugha ya Kikamba maneno haya huchukua kiambishi cha wingi {ma} kama katika neno *sukululenyemaana* ya shule wingi wake ni *masukulu* yaani *mashule*.

Makosa mengine yaliyotambuliwa yalihusu udondoshaji wa fonimu /h/ ambayo ilidondoshwa kwenye mofu ya hali ya mazoea{hu}, kwa mfano *uonekana*, badala ya *huonekana* na *ukosa* badala ya hukosa. Aidha fonimu hii ilidondoshwa pia kwenye kiambishi kikanushi {ha} cha nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili umoja na wingi na nafsi ya tatu umoja na wingi. Kwa mfano *atukutaka* badala ya *hatukutaka*, *ulia* badala ya *hulia*. Kudondosha kwa fonimu /h/ kumefanya mofu hizi kubadilisha umbo pamoja na kupoteza maana. Baada ya uchunguzi, mtafiti alibaini kuwa hali hii ya wanafunzi wa Kikamba kuidondoshwa fonimu /h/ katika hali zilizoelezwa ilitokana na kutokuwepo kwa fonimu hii kwenye mfumo wa kifonolojia wa lugha ya Kikamba. Pia ilibainika kuwa katika lugha ya Kikamba, tofauti na sauti nyingine, fonimu /h/ haina sauti nyingine inayokaribiana nayo, hivyo wanafunzi wanapokumbana nayo huidondosha kabisa katika baadhi ya maneno, na basi kupelekea kuwepo kwa makosa wanapoandika au kutamka maneno ya Kiswahili yenye fonimu hiyo. Baada ya uchunguzi, mtafiti alitambua kuwa kutokana na mifano mingi aliyoweza kuipata, makosa mengi ya uchopekaji, na hata udondoshaji, yalihusu uchopekaji na udondoshaji wa konsonanti /h/. Aidha mtafiti alitambua kuwa hali hii ni kutokana na kutokuwepo kwa fonimu hii katika mfumo wa kifonolojia wa lugha ya Kiswahili na pia kukosekana kwa fonimu inayokaribiana nayo, hivyo wanafunzi hukosa kujua ni wapi waitumie na wapi waiache.

Kando na udondoshaji makosa mengine yalihusu matumizi ya sauti mbadala, ambapo katika matumizi ya lugha ya wanafunzi waliotafitiwa, sauti zisizopatikana katika lugha ya Kikamba ziliondolewa kwenye maneno ya lugha ya Kiswahili na badala yake wakatamia sauti nyingine ambayo ni tofauti kabisa lakini iliyokaribia kufanana na sauti iliyoondolewa. Mathalan, wanafunzi walitumia /l/ badala ya /r/ katika baadhi ya maneno ya Kiswahili, ambayo katika muundo wake, yana sauti /r/. Kwa mfano *walindi* badala ya *waridi*, *linda* badala ya *rinda*. Matumizi mengine ya sauti mbadala yalidhihirika

wanafunzi walipotumia fonimu /mb/ badala ya /b/ kwa mfano *wamembembwa* badala ya *wamebebwawa,sembuleni* badala ya *sebuleni*.

Makosa mengine yalidhihirika katika matumizi ya /s/ badala ya /z/, ambapo baadhi ya maneno ya Kiswahili yenye fonimu /z/, mwanafunzi alitumia fonimu mbadala ya /s/ kwamfano *hasemesekibadala ya hasemezeki,na saidi* badala ya *zaidi, wasasi* badala ya *wazazi*. Hata hivyo mtafiti aligundua kuwa makosa mengi ya ubadala wa sauti yalikuwa katika matumizi ya /mb/ badala ya / b/.

Aidha mtafiti aliweza kupendekeza njia za kukabiliana na makosa ya wanafunzi. Kwanza, kwa kuwataka walimu wanaofunza lugha ya Kiswahili kuwa waangalifu, hasa walioathirika na lugha zao za kwanza wasifanye makosa ambayo huenda wanafunzi wakawaiga. Hivyo basi walimu wanaofundisha lugha ya Kiswahili wanafaa wawe na ujuzi wa hali ya juu wa lugha hiyo ili wanafunzi wao waweze kujifunza vyema na kuwa kielelezo kwao pamoja na kuwakosoa wanafunzi pindi tu wanapofanya makosa. Pia kuna haja ya mwalimukuchunguza vipengele vya L2 vinavyofanana na vya L1 ya mwanafunzi ili amwelekeze namna anavyoweza kuvitumia kusaidia ujifunzaji wake wa L2. Aidha kuna haja ya kuwepo muda zaidi wa somo la Kiswahili ili kuimarisha mtagusano ufaakati ya mwalimu na mwanafunzi.

Kutokana na utafiti huu imebainika wazi kwamba mfumo wa kimofonolojia kati ya lugha ya Kikamba na ile ya Kiswahili ni tofauti licha ya kuwa zote ni lugha za nasaba moja ya Kibantu. Aidha, ni wazi kwamba tofauti hizi zinasababisha wanafunzi wakamba kufanya makosa ya kimofonolojia wanapoandika na hata wanaposoma. Hata hivyo, makosa haya yanaweza kurekebisha iwapo washikadau wote wa sekta ya elimu wakiwemo walimu, wanafunzi na waandalizi wa mitalaa wataweka mikakati ya kukabiliana nayo.

5.3. Mapendekezo

Utafiti huu haukushughulikia makosa yote yanayotokana na athari ya lugha ya Kikamba kwa lugha ya Kiswahili kwa hivyo mtafiti anapendekeza kufanyika kwa tafiti zingine zitakazoangazia viwango vingine vya lugha ambavyo havikushughulikiwa katika utafiti huu vikiwemo sintaksia, semantiki n ahata mofosintaksia. Pia utafiti huu kamwe hauwezi kudai kuwa umeshughulikia mbinu zote za kukabiliana na makosa ya wanafunzi. Hivyo ni maoni ya mtafiti kuwa tafiti zingine zinaweza kufanywa kuhusu mbinu zaidi za kukabiliana na makosa ya mwanafunzi katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Zaidi ya haya ni kuwa utafiti huu umechunguza tofauti za kimofonolojia kama kisababisho kikuu kimojawapo cha makosa kwa hivyo mtafiti anapendekeza tafiti zaidi kufanyika ili kuchunguza vyanzo vingine vya makosa kando na lugha ya kwanza ya mwanafunzi.

Pia, kwa kuwa utafiti huu umeshughulikia lugha ya Kikamba peke yake tafiti nyingine zinaweza kufanywa kuhusu lugha zingine. Aidha ni matumaini ya mtafiti kuwa walimu wanaofunza wanafunzi wenye asili ya lugha ya Kikamba watatilia maanani mikakati aliyopendekeza kama njia za kupunguza makosa wanayofanya wanafunzi wanapojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili.

MAREJELEO

- Al-Badawi, K. (2012). An analysis of phonetic, morphological and syntactic errors in English: A case study of Saudi BA students at King Khalid University. *International Journal of Social Science and Humanity*, 2(6), 536.
- Alonso Alonso, M. R. (1997). Language transfer: Interlingual errors in Spanish students of English as a foreign language. *Revista Alicantina de Estudios Ingleses*, 10, 7–14.
- Booij, G. (2012). *The grammar of words: An introduction to linguistic morphology*. Oxford University Press. <https://books.google.co.ke/books?>
- Brooks, N. (1968). Teaching culture in the foreign language classroom. *Foreign Language Annals*, 1(3), 204–217.
- Brown, D. (2007). *Principles of language learning and teaching* (5th ed.). Pearson.
- Brown, H. D. (2000). *Principles of language learning and teaching* (Vol. 4). Longman New York.
- Bryman, A. (2012). *Social Research Methods 4e*. Oxford University Press.
- Chebet-Choge, S. (2012). Fifty Years of Kiswahili in Regional and International Development. *Journal of Pan African Studies*, 4(10), 172–203.
- Chiraghdin, S., & Mnyampala, M. E. (1978). *Historia ya Kiswahili*. Oxford University Press.
- Chomsky, N. (1957). Fundamentals of Language. *International Journal of American Linguistics*, 23(3), 235–242.
- Chomsky, N. (1961). Some methodological remarks on generative grammar. *Word*, 17(2), 219–239.
- Cook, V. J. (1992). Evidence for multicompetence. *Language Learning*, 42(4), 557–591.
- Corder, S. P. (1967). *The significance of learner's errors*. 4(5), 161–170.

- Corder, S. P. (1993). *Introducing applied linguistics*. Penguin Books.
- Corder, SP. (1981). *Error analysis and interlanguage*. Oxford University Press.
- Corder, Stephen. (1974). *Techniques in applied linguistics*. Oxford University Press.
- Creswell, J. W. (2017). *Designing and Conducting Mixed Methods Research*. SAGE Publications, Incorporated.
- Crystal, D. (1997). *Dictionary of Linguistics and Phonetics*. Blackwell Publishers Ltd.
- Dulay, H. (1982). *Language two*. Oxford University Press.
- Dušková, L. (1969). ON SOURCES OF ERRORS IN FOREIGN LANGUAGE LEARNING. *IRAL - International Review of Applied Linguistics in Language Teaching*, 7(1). <https://doi.org/10.1515/iral.1969.7.1.11>
- Edge, J. (1996). Cross-cultural paradoxes in a profession of values. *Tesol Quarterly*, 30(1), 9–30.
- Ellis, N. C. (1994). Implicit and explicit language learning. *Implicit and Explicit Learning of Languages*, 79–114.
- Ellis, N. C. (2008). *Usage-based and form-focused language acquisition: The associative learning of constructions, learned attention, and the limited L2 endstate*. Routledge/Taylor & Francis Group. <https://psycnet.apa.org/record/2008-07674-015>
- Freeman, D., & Johnson, K. E. (1998). Reconceptualizing the knowledge-base of language teacher education. *TESOL Quarterly*, 32(3), 397–417.
- Fries, C. C. (1945). *Teaching and learning English as a foreign language*. University of Michigan Press.
- Gas, S. (1979). Language transfer and universal grammatical relations. *Language Learning*, 29(2), 327–344.

- Gass, S. M. (2013). *Second language acquisition: An introductory course*. Routledge.
<https://books.google.co.ke/books?>
- Gass, S., & Selinker, L. (2008). *Second language acquisition: An introductory course* (3rd ed.). Routledge.
- Guthrie, M. (1967). *Comparative Bantu; an introduction to the comparative linguistics and prehistory of the Bantu languages*. Gregg.
- Habwe, J., & Karanja, P. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Phoenix Publishers.
- Hartmann, R. R. K., & Stork, F. C. (1972). *Dictionary of language and linguistics*. John Wiley & Sons.
- Herbert, W., Seliger, H. W., Shohamy, E. G., & Shohamy, E. (1989). *Second language research methods*. Oxford University Press. <https://books.google.co.ke/books?>
- Holt, R. (1975). *An Introduction to Language* (2nd ed.). Winston.
- James, C. (1998). *Errors in language learning and use*. Longman.
- Kachipela, D. (2014). *Athari za sheng katika matokeo ya mtihani wa kiswahili katika shule za msingi mtaa wa Kangemi* [PhD Thesis]. University of Nairobi.
- Kamusi la Kiswahili Fasaha. (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Oxford Univ. Press.
- Kamusi ya TUKI. (1990). *Kamusi sanifu ya isimu na lugha*. TUKI : UNESCO : SIDA.
- Kanake, J. K. (2013). *Makosa ya Kifonolojia Miongoni mwa Wanafunzi wa Kiigembe katika Ujifunzaji wa Kiswahili*. Kenyatta University.
- Katamba, F. (1993). *Morphology*. Martin's Press.
- Kattam, R. J. (2016). *Phonological Basis of Misspellings in the Written English of Nandi Students in Eldoret West District* [PhD Thesis, University of Nairobi].
<http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/98653>
- Kerlinger, F. (1986). *Foundations of behavioural research*. Holt.

- Kieti, M. (1988). *Myali song: Social critique among the Kamba* [PhD Thesis, University of Nairobi]. <http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/15575>
- Kihore, Y. (2008). *Stadi za Lugha ya Kiswahili: Sarufi 2*. TUKI.
- Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B., & Msanjila, Y. P. (2003). *Sarufi maumbo ya kiswahili sanifu (SAMAKISA): Sekondari na vyuo*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo kikuu cha Dar es Salaam.
- Kitavi, H. M. (1992). *A comparative study of the Kitui north and Machakos dialects of kikamba* [PhD Thesis, University of Nairobi]. <http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/18216>
- Kitsao, R. (2015). *Uchanganuzi wa makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi na jinsi yanavyochngia matokeo mabaya katika mihani, kata ya Ganze, kaunti ya Kilifi*. Kenyatta University.
- Kothari, C. R. (2004). *Research methodology: Methods and techniques*. New Age International. <https://books.google.co.ke/books?>
- Kothari C. R. (2008). *Research methodology Methods 7 technioques*. New Age International Ltd.
- Krashen, S. D. (1981). *Second Language Acquisition and Second Language Learning*. University of Southern California. <http://ndl.ethernet.edu.et/handle/123456789/58723>
- Lado, R. (1957). *Linguistics across cultures: Applied linguistics for language teachers*. University of Michigan press.
- Lass, R. (1984). *Phonology: An introduction to basic concepts*. Cambridge University Press. <https://books.google.co.ke/books?>

- Littlewood, W., & William, L. (1984). *Foreign and second language learning: Language acquisition research and its implications for the classroom*. Cambridge University Press. <https://books.google.co.ke/books?>
- Macharia, M. (2013). The phonological basis of misspellings in the written English of Kikuyu speakers. *Journal of Language, Technology & Entrepreneurship in Africa*, 4(2), 1–16.
- Mackay, H. (1981). *Mackay Education Report, Report of the National Committee on Educational Objectives and Policies* (pp. 11–12). Government Printer.
- Massamba, D. P. B. (1996). *Phonological theory: History and development*. Dar es Salaam University Press.
- Massamba, D. P. B. (2011). *Maendeleo katika nadharia ya fonolojia*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M., & Hokororo, J. I. (2001). *Sarufi miundo ya Kiswahili sanifu (SAMIKISA): Sekondari na vyuo*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M., & Msanjila, Y. P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili sanifu (FOKISA): Sekondari na vyuo*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mathooko, P. (2004). *Towards integrative perspective of linguistic accommodation: A case study of Kikamba and Kitharaka*. Kenyatta University.
- Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya lugha isimu na nadharia: Kwa sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu*. Serengeti Educational Publishers Limited.
- Mbula, E. (2011). *Uchanganuzi wa makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa kikamba wanapojifunza Kiswahili sanifu* [Thesis, University of Nairobi]. <http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/3307>

- Mgullu, R. (1999). *Mtala wa isimu: Fonetiki, fonolojia na morfolojia ya Kiswahili*. Longhorn.
- Mgullu, R. S. (1990). *The structure of Kiswahili sentences: A transformational generative approach* [PhD Thesis]. University of Dar es Salaam.
- Miller, G. A. (1966). Language and Psychology. In *New Directions in the Study of Language*. M. I. T. Press.
- Moeller, A. K., & Catalano, T. (2015). Foreign language teaching and learning. *International Encyclopedia of the Social & Behavioral Sciences*, 327–333.
- Mohammed. (2011). *Assimilation in English Connected Speech*. iasj.net. <https://www.iasj.net/iasj/download/49a5290116353f98>
- Mudhune, E. (1994). *A Contrastive Analysis Approach to the learning of Swahili Morphosyntax by Luo Learners*. Kenyatta University.
- Mulokozi, M. M. (2002). *Kiswahili as a national and international language*. Institute of Kiswahili Research.
- Musau, P. M. (1993). *Aspects of interphonology: The study of Kenyan learners of Swahili*. Bayreuth University.
- Mutiga, J. M. (2002). *The tone system of Kikamba: A case study of Mwingi dialect* [PhD Thesis]. University of Nairobi.
- Mwita, L. (2009). The adaptation of Swahili loanwords from Arabic: A constraint-based analysis. *The Journal of Pan African Studies*, 8(2), 46–60.
- Mwove, A. (1987). *The Kikamba noun phrase*. University of Nairobi.
- Ndeti, K. (1972). *Elements of Akamba*. East Africa Publishing House.
- Nganga. (2002). *Makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi na jinsi yanavyoshughulikiwa na walimu katika tarafa ya Maragwa*. University of Nairobi.

- Nida, E. A. (1949). *Morphology: The descriptive analysis of words*. University of Michigan Press.
- Norrish, J. (1987). *Language Learning and Their Errors*. Macmillan Publisher.
- Ntawiyanga, S. (2014). *Changamoto za Kimofosintaksia Miongoni Mwa Wanafunzi wa Kiswahili wa Shule za Upili Wilayani Muhanga, Nchini Rwanda* [Kenya University]. <https://ir-library.ku.ac.ke/handle/123456789/10782>
- Obara, J. M. (2014). *Uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii* [PhD Thesis]. University of Nairobi.
- Odlin, T. (1989). *Language transfer: Cross-linguistic influence in language learning*. Cambridge University Press.
- Otiende, M. A. (2013). *Athari za kimofonolojia za kiolusuba katika matumizi ya kiswahili sanifu kama lugha ya pili* [PhD Thesis]. University of Nairobi.
- Polomé, E. C. (1967). *Swahili language handbook*. Center for Applied Linguistics.
- Posner, R. (1975). *Morphology. An Introduction to the Theory of Word-Structure*. JSTOR.
- Punch, K. F., & Oancea, A. (2014). *Introduction to research methods in education* (2nd ed.). SAGE. <https://books.google.co.ke/books?>
- Richards, J. C. (1974a). A non-contrastive approach to error analysis. *Error Analysis: Perspectives on Second Language Acquisition*, 172–188.
- Richards, J. C. (1974b). A non-contrastive approach to error analysis. *Error Analysis: Perspectives on Second Language Acquisition*, 172–188.
- Richards, J. C., & Schmidt, R. W. (2002). *Longman Dictionary of Language Teaching and Applied Linguistics*. Routledge.
- Schane, S. A. (1973). *Generative phonology*. Prentice-Hall.

- Schumann, J. H., & Stenson, N. (1974). *New Frontiers in Second Language Learning*. Newbury House.
- Selinker, L. (1972). *Interlanguage*. Rowlence Eribaum Associates.
- Selinker, L., & Gass, S. M. (1992). *Language transfer in language learning*. John Benjamins Publishing Company. <https://www.semanticscholar.org>
- Selinker, L., & Gass, S. M. (2008). *Second language acquisition* (2nd ed.). Lawrence Earlbaum Associates.
- Shalaby, N. A., Yahya, N., & El-Komi, M. (2009). Analysis of lexical errors in Saudi college students' compositions. *Journal of the Saudi Association of Languages and Translation*, 2(3), 65–92.
- Shiundu, J., & Omulando, J. (1992). *Current Theory and Practice in Kenya*. Nairobi. Oxford University Press.
- Waweru, M. M. (2012). *Lexical and phonological errors in the spoken English language of pre-school teachers in classrooms in Kasarani division* [Thesis, University of Nairobi]. <https://ir-library.ku.ac.ke/handle/123456789/2496>
- Whiteley, W. H., & Muli, M. G. (1962). *Practical introduction to Kamba*. Oxford University Press.

Kiambatanisho 1: Fomu ya hiari ya kushiriki utafiti

SEHEMU YA KWANZA: HABARI KUHUSU MTAFITI

Jina langu ni Victoria Kalungu mwanafunzi wa shahada ya uzamili kutoka Chuo Kikuu cha Pwani nambari ya usajili C50/PU/3032/14. Wasimamizi wangu ni Dkt Nancy Ngoa na Dkt Justus Chimoni. Utafiti wangu unahusu *Uchanganuzi wa makosa ya kimofonolojia katika lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wenye asili ya lugha ya Kikamba*. Data ya utafiti huu inakusanywa kutoka kaunti ya Makueni.

Umuhimu wa Utafiti

Lugha ya Kiswahili inatekeleza majukumu muhimu hapa nchini Kenya. Kwanza Kiswahili ni lugha ya taifa na pia lugha rasmi. Aidha Kiswahili ni mojawapo ya masomo ya lazima katika shule za msingi na upili. Zaidi ya hayo lugha hii imevuka mipaka na kwa sasa ni mojawapo wa lugha zinazotambulika ulimwenguni. Hata hivyo, lugha hii inakabiliwa na changamoto nyingi mojawapo ikiwa athari ya lugha za kwanza ikiwemo lugha ya Kikamba. Ndiposa utafiti huu unanua kuchunguza athari za kimofonolojia ya lugha ya Kikamba kwa lugha ya Kiswahili ili kupendekeza njia za kuzitatua athari hizo na kuwezesha lugha ya Kiswahili kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Umechaguliwa kushirikishwa katika utafiti huu kama mtafitiwa kwa sababu utafiti unalenga wanafunzi wanaozungumza Kikamba kama lugha yao ya kwanza. Maandishi yako na rekodi yako itatunzwa kwa njia ya siri na mtafiti. Aidha kushiriki kwako ni juu ya hiari yako. Hata hivyo, mtafiti atajivunia kushiriki kwako katika utafiti huu.

SEHEMU YA PILI: UNGAMO LA KUSHIRIKI UTAFITI

Nathibitisha kwamba nimesoma taarifa zilizopo hapa juu na kuzielewa na kuhiari kushiriki katika utafiti huu.

Jina la mtafitiwa.....

Sahihi.....

Tarehe.....

Kiambatanisho 2: Mada ya insha itakayotolewa kwa wanafunzi

Umepewa dakika arubaini. Andika insha ya ukurasa mmoja yenye mada;

Siku iliyofana sana

Isome kwa sauti insha uliyoiandika